PARLIAMENT OF TANZANIA • BUNGE LA TANZANIA •

Jarida la BUNGE

ISSN-085-6046 TOLEO LA KUMI NA TATU SEPTEMBA, 2026




# "Mkutano wa IPU Kufanyika Jijini Arusha


## Oktoba 5 hadi 9, 2026

### Washiriki 2,000 Kuhudhuria"

**Bunge lathibitisha uteuzi wa Ndejembi**



UK. 07



**Spika Azindua Maadhimisho Ya Miaka 100 Ya Bunge** UK. 11



**Mkutano wa 55 wa CPA Kanda ya Afrika** UK. 22



**Ukuaji na Maendeleo ya Sekretarieti ya Bunge la Tanzania** UK. 40

*Scan hii Code kusoma na kupakua jarida hili*

# Dibaji



Ndugu Msomaji,

Toleo hili la Kumi na Tatu la Jarida la Bunge linakuja wakati ambapo Bunge la Tanzania litakuwa na matukio mawili makubwa ya kihistoria.

Kwanza, ni kuhusu Bunge kuwa mwenyeji wa Mkutano wa 153 wa Umoja wa Mabunge Duniani (IPU), utakaofanyika Oktoba 5-9 Jijini Arusha. Katika Toleo hili, ipo habari kuhusu Mkutano wa Wahariri wa Vyombo vya Habari na Mhe. Mussa Azzan Zungu, Spika wa Bunge (Mb) akizungumzia Mkutano huo utakaowakutanisha zaidi ya washiriki 2000 kutoka Mataifa 183 Duniani.

Pili, ni kuhusu uzinduzi wa Maadhimisho ya Miaka 100 ya Chimbuko la Bunge la Tanzania. Katika Historia ya Bunge, mwaka huu linatimiza karne moja tangu lilipoanzishwa mwaka 1926 wakati huo likiitwa Baraza la Kutunga Sheria la Tanganyika.

Hivyo, ipo habari inayohusu uzinduzi wa maadhimisho hayo adhimu ambayo yamelenga kusherehekea mageuzi ya demokrasia ya kibunge nchini Tanzania, kwa kufuatilia historia yake kutoka mifumo ya utawala wa kikoloni hadi sasa.

katika Jarida hili pia, kuna habari kuhusu Mkutano wa 55 wa Chama cha Mabunge ya Jumuiya ya Madola (CPA), Kanda ya Afrika uliofanyika Jijini Lilongwe, Malawi na Mkutano wa Ngazi ya Juu wa Umoja wa Mataifa kuhusu Malengo ya Maendeleo Endelevu (HLPF) uliofanyika Jijini New York, Marekani.

Aidha, Habari nyingine ni kuhusu hutoba iliyotolewa na Waziri Mkuu wakati wa kuahirishwa kwa Mkutano wa Tatu wa Bunge, habari kuhusu Vikao vya Kamati za Kudumu za Bunge, Miswada iliyopitishwa na Bunge pamoja na habari kuhusu maonesho mbalimbali ambayo Ofisi ya Bunge imeshiriki. Mbali na hayo Jarida hili lina Makala za uchambuzi kuhusu masuala mbalimbali ya kibunge.

Nawatakia usomaji mwema wa Jarida la Bunge.

**Ndugu Baraka Leonard**
**Katibu wa Bunge.**


## BODI YA UHARIRI

**Mwenyekiti**
Ndg. Baraka Leonard

**Makamu Mwenyekiti**
Ndg. Zuhura Mtatifikolo

**Wajumbe**
Ndg. Athuman Hussein, *ndc*
Ndg. Hanifa Masaninga
Ndg. Abdallah Hancha
Ndg. Chacha Nyakega

**Mhariri**
Ndg. Lawrence Raphaely

**Mhariri Msaidizi**
Ndg. Debora Sanja

**Msanifu Kurasa**
Henry Mbilinyi




Ofisi ya Bunge,
10 Barabara ya Morogoro
S.L.P. 941,
40490 Tambukareli,
DODOMA.
Nukushi: +255 26234218
Simu: +255 26 232276-5
Barua Pepe: cna@bunge.go.tz


*Scan hii Code kusoma na kupakua jarida hili*



# Yaliyomo


Washiri zaidi ya 2000 kushiriki mkutano wa IPU — UK. 02

Bunge lathibitisha uteuzi wa Ndejembi — UK. 07

Spika Azindua Maadhimisho ya Miaka 100 ya Bunge — UK. 11

Waziri Mkuu Akemea Usumbufu kwa Wajasiriamali — UK. 18

Mkutano wa 55 wa CPA Kanda ya Afrika Wafanyika. — UK. 22

Spika Ashiriki Mkutano wa Jukwaa La Kibunge-Marekani — UK. 26

Bunge Lapitisha Miswada Mitano ya Sheria — UK. 28

Naibu Spika Sillo: Tanzania Inatekeleza kwa Ufanisi Ajenda 2063 ya AU — UK. 30

LAAC na PAC zahoji Wizara, Taasisi na Halmashauri Matumizi ya Fedha — UK. 32

Ofisi ya Bunge Yashiriki Maonesho Mbalimbali — UK. 34

Mfahamu Randhir Thaker na Uhusiano Wake na Bunge — UK. 38

Ukuaji na Maendeleo ya Sekretarieti ya Bunge la Tanzania — UK. 40

Hoja Kuhusu Utaratibu Bungeni: Ulinzi wa Mjadala, si Kumkatiza Mbunge — UK. 47

Ndoto ya Sheria Ndogo: Safari ya Kutafuta Dhamira ya Bunge katika Mamlaka Yaliyokasimiwa — UK. 51

Hoja za Ukaguzi: Maswali Hadi Majibu - Uwajibikaji Bungeni — UK. 55

Maswali ya Wabunge: Sauti ya Wananchi Bungeni — UK. 58




# Washiriki 2,000 Kuhudhuria Mkutano Wa IPU Jijini Arusha

**Rais Samia kufungua mkutano huo Jijini Arusha**

**"Tanzania kuwa mwenyeji wa Mkutano wa 153 ni sehemu ya ratiba ya kawaida ya IPU, lakini ni fursa kubwa kwa nchi kwa sababu mkutano huo huleta pamoja mamia ya wabunge na viongozi kutoka dunia nzima," alisema.**

Na *Zuhura Mtatifikolo*

Tanzania inatarajia kupata fursa kubwa za kiuchumi, utalii, uwekezaji na kuimarisha diplomasia ya kimataifa kupitia Mkutano wa 153 wa Umoja wa Mabunge Duniani (IPU), unaotarajiwa kufanyika jijini Arusha kuanzia Oktoba 5 hadi 9, 2026.

Mkutano huo unaotarajiwa kuwakutanisha takribani washiriki 2,000 kutoka mabunge mbalimbali duniani, unatajwa kuwa jukwaa muhimu kwa Tanzania kuionesha dunia fursa zilizopo katika sekta za Utalii, Biashara na Uwekezaji, sambamba na kujenga mahusiano mapya ya kimataifa.

Taarifa hiyo imetolewa na Spika wa Bunge, Mhe. Mussa Azzan Zungu wakati akizungumza na waandishi wa habari Agosti 4, 2026 katika Kituo cha Kimataifa cha Mikutano (AICC) Jijini Arusha kuhusu utayari wa Bunge kuwa mwenyeji wa mkutano huo.

Alisema Mkutano huo wa kihistoria utafunguliwa rasmi na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, tarehe 5 Oktoba, 2026.

"Kawaida mikutano kama hii huwa inafanyika








mara mbili kwa mwaka kipindi cha Machi/Aprili na mwingine hufanyika kipindi cha Oktoba, hivyo Tanzania kuwa mwenyeji wa Mkutano wa 153 ni sehemu ya ratiba ya kawaida ya IPU, lakini ni fursa kubwa kwa nchi kwa sababu mkutano huo huleta pamoja mamia ya wabunge na viongozi kutoka nchi wanachama," alisema.

Mhe. Mussa alisema Tanzania inajivunia kuwa mwenyeji wa mkutano huo na kwamba ni fursa ya kipekee kwa nchi kuonesha uwezo wake wa kuandaa mikutano mikubwa ya kimataifa, pamoja na kuonesha amani, utulivu na ukarimu wa Watanzania.

Akizungumza kuhusu maandalizi ya mkutano huo, Mhe. Zungu alisema ujio wa viongozi wa mabunge, wabunge, wanadiplomasia na wadau mbalimbali kutoka sehemu tofauti za dunia utatoa nafasi kwa Tanzania kujitangaza zaidi katika sekta ya utalii na uwekezaji.

"Hii inadhihirisha wazi imani kubwa ambayo Jumuiya ya Kimataifa ya Mabunge inayo kwa nchi yetu na inathibitisha dhamira yetu ya muda mrefu katika kudumisha demokrasia, amani, ushirikiano wa Kimataifa na Diplomasia ya Kibunge"

"Bunge la Tanzania limejiandaa kikamilifu kuwa mwenyeji wa Mkutano wa 153 wa IPU hii ni heshma kubwa kwa nchi yetu na pia ni fursa muhimu ya kiuchumi, diplomasia na kitamaduni ambayo itaongeza hadhi ya nchi katika medani za kimataifa". alisema,

Kwa mujibu wa Spika Zungu, wageni watakaofika nchini watapata nafasi ya kushuhudia vivutio mbalimbali, utamaduni na ukarimu wa Watanzania, jambo ambalo linaweza kuwa kichocheo cha kuongeza idadi ya watalii na wawekezaji watakaovutiwa kuja nchini.

Alisema Mkutano huo utafanyika katika Jiji la Arusha ambalo ni moja ya miji muhimu ya mikutano na utalii nchini Tanzania.

Alisema Jiji hilo pia lina ukaribu na baadhi ya vivutio vikubwa vya utalii ikiwemo Mlima Kilimanjaro, Hifadhi ya Taifa Serengeti na Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro.

Mhe. Zungu alitoa wito kwa wajumbe wa mkutano kutumia muda wao kutembelea vivutio na urithi wa kitamaduni wa Tanzania.

*Jarida la* Bunge | Toleo la Kumi na Tatu Septemba 2026

> *Mkutano huo pia utakuwa muhimu katika kuimarisha diplomasia ya kibunge na uhusiano wa Tanzania na mataifa mengine*
>
> *- Spika Mussa Azzan Zungu*

## Fursa kwa wafanyabiashara

Mbali na utalii, alisema mkutano huo unatoa fursa kwa wafanyabiashara wa ndani kupitia ongezeko la mahitaji ya huduma mbalimbali wakati wa mkutano.

"Sekta za hoteli, usafirishaji, migahawa, huduma za mikutano, mawasiliano na huduma nyingine zinazohusiana na wageni zinatarajiwa kunufaika kutokana na uwepo wa maelfu ya washiriki.

"Kwa Tanzania, hii ni nafasi ya kuhakikisha wafanyabiashara wanatumia ujio wa wageni hao kujenga mahusiano ya kibiashara na kutangaza bidhaa na huduma zinazozalishwa nchini," alisema.

Aidha, alisema wageni kutoka nchi mbalimbali wanaweza kuwa mabalozi wa Tanzania watakaporejea katika mataifa yao, hasa baada ya kupata uzoefu wa moja kwa moja kuhusu mazingira ya biashara, utalii na utamaduni wa Tanzania.

## Uimarishaji wa Diplomasia

Spika Zungu alisema mkutano huo pia utakuwa muhimu katika kuimarisha diplomasia ya kibunge na uhusiano wa Tanzania na mataifa mengine.

Mkutano huo utafanyika chini ya kaulimbiu "Kuimarisha Utawala Bora na Kuiwezesha Jamii kupitia Ushirikishwaji, Imani na Fursa kwa Wote".

"Kwa mujibu wa IPU, mjadala mkuu utatoa nafasi kwa wajumbe kujadili utawala bora, ushirikishwaji na hatua za kibunge katika kuwawezesha wananchi," alisema.

Mhe. Zungu alisema diplomasia ya kibunge ina nafasi muhimu katika kujenga madaraja ya maelewano kati ya mataifa kupitia mazungumzo, ushirikiano na kubadilishana uzoefu.

Alisema Tanzania inapaswa kutumia fursa hiyo kuimarisha uhusiano na mabunge mengine duniani na kuendelea kujenga taswira yake kama nchi inayothamini amani, demokrasia na ushirikiano wa kimataifa.

## Masuala ya Dunia Kujadiliwa

Mhe. Spika alisema mbali na hayo pia mkutano huo utajadili changamoto mbalimbali zinazoikabili dunia, zikiwemo utawala wa kidemokrasia, amani na usalama, mabadiliko ya tabianchi, teknolojia na akili unde, pamoja na ushiriki wa wanawake, vijana na watu wenye ulemavu.

Alisema miongoni mwa mambo mengine watakayoyajadili ndani ya mkutano huo ni pamoja na Kamati za Kudumu, Jukwaa la Wanawake Wabunge na Jukwaa la Wabunge Vijana.

"Majadiliano hayo ni muhimu kwa sababu dunia ya sasa inakabiliwa na changamoto zinazohitaji ushirikiano wa mataifa badala ya kila nchi kufanya kazi peke yake.

"Diplomasia ya kibunge inaweza kusaidia kujenga uelewano na kutafuta suluhisho la changamoto kupitia majadiliano na makubaliano," alisema.



## Mhe. Dkt. Tulia Ackson kuongeza heshima

Mhe. Zungu alisema mkutano huo unafanyika wakati Tanzania ikiwa na nafasi ya kipekee ndani ya IPU kupitia Spika wa Bunge Mstaafu Mhe. Dkt. Tulia Ackson (Mb), ambaye ni Rais wa Umoja huo.

Alisema uongozi wake umeongeza uzito wa Tanzania katika diplomasia ya kibunge na kutoa




nafasi kwa nchi kuendelea kuonekana katika majukwaa ya kimataifa.

"Umoja wa Mabunge Duniani ulioanzishwa mwaka 1889 ni moja ya taasisi kongwe ya kimataifa wenye Dira inayosema 'Tunataka kuwa na dunia ambayo kila sauti ina thamani, ambayo demokrasia na mabunge yanatumikia watu kwa ajili ya amani na maendeleo'

"Ni jambo la kujivunia kuwa, Mtanzania mwenzetu Mhe. Dkt. Tulia Ackson (Mb) ndiye Rais wa IPU kwa sasa, nafasi ambayo ameishika tangu mwaka 2023 na kuitumikia vema katika kuhakikisha ufanikishaji wa dira hiyo," alisema.

Kwenye Mkutano wa 153 IPU, Baraza la Uongozi linatarajiwa kusimamia uchaguzi wa Rais mpya wa Umoja huo wakati wa kikao kitakachofanyika Arusha.

### Maandalizi kukamilika kwa wakati

Mhe. Zungu alisema maandalizi ya mkutano yanaendelea vizuri kwa ushirikiano kati ya Bunge la Tanzania, Serikali, Sekretarieti ya IPU na wadau wengine.

"Maandalizi hayo yanahusisha usalama, usafirishaji, malazi, usajili, huduma za afya, tafsiri na mahitaji ya vyombo vya habari.

"Kwa Tanzania, mafanikio ya mkutano huo yatapimwa si kwa namna utakavyofanyika pekee, bali pia kwa fursa zitakazobaki baada ya wageni kuondoka nchini," alisema

Mhe. Zungu alisema iwapo fursa hizo zitatumiwa vizuri, mkutano utakuwa kichocheo cha kuongeza utalii, kuvutia wawekezaji, kufungua milango ya biashara na kuimarisha mahusiano ya Tanzania na mataifa mengine.

"Wakati maandalizi yakielekea kukamilika, matarajio si tu Tanzania kuwa mwenyeji mzuri wa mkutano, bali kutumia jukwaa hilo kuonesha dunia kwamba Tanzania ni mahali salama kwa mikutano, utalii, biashara na uwekezaji," alisema.

Alieleza kuwa Mkutano wa 153 wa IPU ni zaidi ya mkutano wa wabunge kwa kuwa ni fursa ya Tanzania kujitangaza, kujenga mahusiano mapya na kutumia diplomasia ya kibunge kama daraja la kufungua milango mipya ya maendeleo ya taifa.







# Bunge lathibitisha uteuzi wa Ndejembi, apata kura zote za ndiyo

Wabunge waliokuwa ndani ya Ukumbi wakati wa upigaji wa kura kwenye mchakato huo, **walikuwa 324**

**Kura zote zilikuwa za ndiyo** bila kura kuharibika wala iliyosema hapana.

*Na Zuhura Mtatifikolo,*

Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania limethibitisha uteuzi wa Makamu wa Rais Mhe. Deogratius Ndejembi kwa kura 324 sawa na asilimia 100 za Wabunge waliokuwepo ukumbini.

Wabunge waliokuwa ndani ya Ukumbi wakati wa upigaji wa kura kwenye mchakato huo, walikuwa 324 na kura zote zilikuwa za ndiyo bila kura kuharibika wala iliyosema hapana.



## Nyadhifa Alizopitia

**2016 - 2020**
**Mkuu wa Wilaya** -Wilaya ya Kongwa

**2020 - Sasa**
**Mbunge -** Jimbo la Chamwino

**2020 - 2024**
**Naibu Waziri -** Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora.

**2024 - 2025**
**Waziri -** Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi

**2024 - 2026**
**Waziri -** Nishati

> **“Mhe. Ndejembi ni mtu mnyenyekevu, mtiifu, mchapakazi na asiyetiliwa shaka kwenye utumishi wake”**
>
> Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. **Mwigulu Nchemba**

Spika wa Bunge Mhe. Mussa Zungu (Mb) alisema matokeo hayo yanatuma ujumbe kwa Rais kuwa, wabunge wanampenda na wana imani naye ndiyo maana wamethibitisha kwa kura zote jina lililoletwa kwa ajili ya kumpata msaidizi wake.

“Wingi wa kura hizo umethibitisha imani ya Wabunge kwa Makamu wa Rais ambaye alikuwa Mbunge mwenzetu, lakini kwa Mhe. Rais Dk Samia Suluhu Hassan ambaye ndiye aliyependekeza jina hili ili kumpata msaidizi wake,” alisema Mhe. Zungu.

Katika maneno yake kabla na baada ya kupigwa kura, Spika Mhe. Zungu alisema kazi iliyo mbele ya Makamu wa Rais ni kuhakikisha anakwenda kuwa msaada kwa Rais na kumuondoa mawazo katika kutimiza majukumu ya kuwatumikia wananchi.

Uteuzi na hadi kupigiwa kura za Wabunge kwa Mhe. Ndejembi umekuja kufuatia kujiuzulu katika nafasi hiyo kwa aliyekuwa Makamu wa Rais Mhe. Dkt. Emmanuel Nchimbi ambaye pia chama chake cha CCM kimemfuta uanachama.

Mapema Ijumaa ya Agosti 28,2026 Rais Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan kupitia kwa Katibu wake Balozi Ali Jabir Mwadini akiwa ameambatana na Mpambe wa Rais Brigedia Jenerali Nyamburi Mashauri waliwasilisha jina la Mhe. Ndejembi kwa ajili ya mchakato wa kuthibitishwa na Bunge.







Ndani ya Ukumbi wa Bunge, Mhe. Spika Mussa Zungu (Mb) alilitaja jina la Mhe. Ndejembi na kufanya ukumbi kulipuka kwa shangwe na nderemo kutoka kwa Wabunge ishara iliyoonyesha aliyependekezwa ni mtu aliyekubalika na wote ikiwemo kundi la wabunge waliowachache.

Akisoma wasifu wa mteule huyo, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Mwigulu Nchemba amemtaja Mhe. Ndejembi kuwa mtu mnyenyekevu, mtiifu, mchapakazi na asiyetiliwa shaka kwenye utumishi wake.

Mhe. Dk Mwigulu alibainisha hayo wakati akitoa hoja ya Bunge ili kuthibitisha jina hilo kwa nafasi ya mtu ambaye atakuwa msaidizi wa kwanza kwa Rais.

Kwa mujibu wa Ibara ya 47(1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Makamu wa Rais ndiye msaidizi mkuu wa Rais kuhusu masuala yote ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mbunge wa Geita Vijijini Joseph Kasheku Musukuma amemwelezea Makamu wa Rais Mhe. Deogratius Ndejembi kwamba ni rafiki wa kila mtu na katika utumishi wake hajawahi kumpigisha ‘shoti’ mtu mwingine ili yeye apate cheo.

“Huyu Mhe. Ndejembi ni kijana mdogo, lakini ni kiongozi mwenye uwezo na maono makubwa, amepata nafasi hii kwa mapenzi ya Mungu na uwezo wake lakini hajawahi kumpigisha mtu mwingine shoti ili kusudi yeye apate cheo,” amesema Musukuma alipounga mkono hoja ya Waziri Mkuu.

Mbunge huyo anasema kuwa waliambatana na Mhe. Ndejembi nchini Marekani na kwamba wakati anapokea ujumbe wa uteuzi, walikuwa pamoja kwenye Ubalozi wa Tanzania nchini humo wakati huo mteule alikuwa amekaa mbele akiwatambulisha watu alioambatana nao kwenye msafara huo.

Mbunge mwingine ambaye amechangia kwenye hoja hiyo, alikuwa ni Mhe. Elibariki Kingu ambaye alimmwagia sifa Mhe. Ndejembi akimtaja kama mtu mchapakazi, mwenye uzalendo ndani yake na mwenye uwezo wa kuring’arisha Taifa na Bunge.

Kingu anasema kuwa Taifa limepata kijana mwenye kaliba ya unyenyekevu na kujishusha kwa kila mtu na nidhamu katika kazi anazozifanya kila siku lakini akamuomba Mhe. Ndejembi kusimama imara kwa ajili ya kumsaidia Rais.

Mwenyekiti wa Wabunge wa Mkoa wa Dodoma Mhe. George Simbachawene amemtaja Makamu

wa Rais kama kijana mvumilivu, mwenye mipango thabiti anayeweza kujitoa kwa ajili ya nchi yake.

Mhe. Simbachawene anasema Ndejembi anaweza kupatikana kwa urahisi zadi na katika mazingira sahihi lakini ni mtu ambaye anapenda kusikiliza na kujifunza kwa wenzake pia.

Katika mchango wake kwenye hoja hiyo, Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge, Uratibu na Wenye Ulemavu Mhe. Prof. Palamagamba Kabudi, amemuomba Makamu wa Rais kuwa mtii na mnyenyekevu tena asinyanyue mabega kuzidi yule aliyemteua ili amsaidie kwenye nafasi hiyo.

"Wewe ni mwanangu ingawa kuanzia leo hauwi mwanangu tena bali kiongozi wangu, nakusihi uendelee kuwa na utii usiokuwa na mashaka, uwe na staha, rizika na kutunza ulichopewa ili kisikupite," amesema Parofesa Kabudi.

Waziri Profesa Kabudi pia amesoma ujumbe wa wazee wa Kabila la Wagogo ndani ya ukumbi akieleza namna walivyomtaka akajinyenyekeze katika majukumu yake na kumsaidia Rais hasa katika kipindi hiki ambacho Taifa linapita kwenye mambo mengi.

Mbunge wa Segerea Mhe. Agnesta Lambati alisema licha ya yeye kuwa upande wa wabunge walio wachache, lakini anayo imani kubwa na Mhe. Ndejembi na kwamba uteuzi wake ni sahihi akisema lazima angempa kura na akaomba na wengine kumpigia kura za ndiyo.

Akizungumzia shangwe la wabunge, Mbunge wa Bukombe na Naibu Waziri Mkuu Mstaafu Mhe. Dkt. Doto Biteko amesema jina lilianzia kwa Wajumbe wa Kamati Kuu ya Halmashauri Kuu ya CCM ambao baada ya kupokea jina hilo kutoka kwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan walilipuka kwa shangwe na nderemo hali iliyoonesha hakuna mashaka kwa Mbunge huyo wa Chamwino.

Kwa mujibu wa Mhe. Biteko, sifa mojawapo ya Makamu huyo wa Rais ni kumsikiliza mtu kwa umakini ili aweze kumuelewa siyo kuharakisha kutafuta majibu ya kumpa mtu.

Wabunge wengine waliochangia kwenye hoja ya Waziri Mkuu na kuunga mkono ni Mhe. Rashid Shangazi, Mhe. Keneth Nollo, Mhe. Tauhida Gallos, Mhe. Hussein Bashe, Mhe. Ali King, Waziri wa Madini Mhe. Anthony Mavunde, na Mhe. Ahmed Shabiby.

Katika ufafanuzi wake, Mwanasheria Mkuu wa Serikali Mhe. Hamza Johari alisema hakuna mahali ambapo Katiba imevunjwa kama ambavyo baadhi ya watu walikuwa wakieneza kwenye mitandao ya kijamii.

Mhe. Johari anasema kila hatua kwenye mchakato huo ilikuwa imezingatiwa na kufuata misingi ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tangu kujiuzuru kwa mtangulizi wa Mhe. Ndejembi, Dkt. Emmanuel Nchimbi.

### Mhe. Ndejembi alivyowashukuru Wabunge

Mara baada ya kupigiwa kura na kuhesabiwa, amesema imani aliyopewa na Mhe. Rais haikuanzia hapa bali amekuwa akimuamini kwa muda mrefu na kumteua kwa nafasi za Waziri katika Wizara mbalimbali kabla ya hapo.

Mhe. Ndejembi anasema dhamana yake haitapimwa kwa ujana wake bali kwa kazi alizotumwa na mamlaka.

"Nakwenda kuwa Makamu wa Rais wa Watanzania wote, kwa Mbunge Sigrada, kwa ndugu yangu Ado Shaibu na kwa Shingo ambao ni wapinzani, siwi Makamu wa wananchi wa CCM pekee,"alisema Ndejembi.

Ndejembi anasema atajitahidi kumsaidia Mhe. Rais na atakuwa kiungo mzuri huku akizingatia kuwa amekopeshwa imani na utu na anatakiwa kulipa hivyo.

Waziri huyo wa zamani wa Nishati amewamwagia sifa wabunge kwa jinsi walivyompa ushirikiano na hata namna walivyompatia kura kwa uaminifu usiotiliwa shaka na kuonesha kweli walijenga imani kwake.

Kingine aliwaomba wananchi wa Jimbo lake la Chamwino kutokumtenga kwani bado ni mwenzao na kwamba kila watakaloona linafaa kumshirikisha wasisite kufanya hivyo naye atakuwa tayari kuwasaidia.







# Spika Azindua Maadhimisho ya Miaka 100 ya Bunge



BUNGE LA TANZANIA
MIAKA 100
HISTORIA YETU, DIRA YETU
1926 - 2026

*Na Debora Sanja*

**Spika wa Bunge Mhe. Mussa Azan Zungu amesema wakati Bunge likiwa linatimiza miaka 100 tangu chimbuko lake, limeendelea kuwa imara katika kutekeleza wajibu wake kwa mujibu wa Katiba ya Tanzania.**

Mhe. Spika alitoa kauli hiyo, wakati akizungumza na Waharir wa Vyombo vya Habari Julai 1, 2026 jijini Dar es Salaam katika uzinduzi wa Maadhimisho ya miaka 100 ya Chimbuko la Bunge la Tanzania.

Alisema tangu Bunge la Kwanza hadi Bunge hili la Kumi na Tatu, hakuna Bunge ambalo limekuwa bora zaidi ya lingine na kwamba mabunge yote ni imara na yanatimiza wajibu wake.

"Hatusemi kwamba Bunge ni dhaifu na hakuna Bunge lililokuwa bora zaidi ya lingine, kazi ya mabunge yote ni ustawi wa jamii.

"Ndio maana Bunge limefanya maboresho kwa kutumia Kanuni ya 5 ambapo Spika anaweza kufanya uamuzi kwa kurejea uamuzi wa maspika wengine waliopita au mabunge mengine ikiwa jambo hilo halijatajwa katika Katiba, Kanuni au muongozo wowote," alisema.

Alisema kwa sasa kunaweza kusiwe na mijadala mikali Bungeni kutokana na maendeleo makubwa yaliyofanywa na Serikali ikiwemo ujenzi wa shule, miundombinu mbalimbali pamoja na kuboreshwa kwa huduma za afya kote nchini.

"Hivyo, mwaka 2026 ni mwaka wa kihistoria wa kuadhimisha miaka 100 ya taasisi hii muhimu katika maendeleo ya taifa letu. Maadhimisho haya yataongozwa na kauli mbiu inayosema **"Miaka 100 ya Bunge: Historia Yetu, Dira Yetu,"**




**"Aliyataja mafanikio mengine kwamba ni kuongezeka kwa matumizi ya mifumo ya kidijitali katika shughuli za Kibunge, kuimarika kwa diplomasia ya Kibunge kupitia ushiriki wa Tanzania katika Mikutano mbalimbali ya Kikanda na Kimataifa, kuongezeka kwa uwazi katika shughuli za Bunge na kuendelea kwa maboresho ya miundombinu na mazingira."**





"Maadhimisho haya yatatoa fursa ya kutafakari historia ya Bunge, kutambua mchango wa viongozi mbalimbali pamoja na kuweka dira ya Bunge kwa miaka mingine ijayo." alisema Mhe. Spika.

### Nafasi ya Bunge katika Demokrasia na Maendeleo ya Taifa

Mhe. Spika alisema Bunge ni chombo kikuu cha uwakilishi wa wananchi ambacho kina jukumu la kutunga sheria, kuishauri na kuisimamia Serikali na kuwawakilisha wananchi.

Alisema kupitia majukumu hayo, Bunge limekuwa mhimili muhimu katika kuimarisha demokrasia, utawala bora na maendeleo ya kiuchumi na kijamii.

"Sheria mbalimbali zinazopitishwa na Bunge zimewezesha kuimarika kwa mazingira ya uwekezaji, utoaji wa huduma za jamii na usimamizi wa rasilimali za Taifa," alisema.

"Vilevile, Bunge limeendelea kuimarisha ushirikiano na wananchi kupitia Kamati za Bunge, mikutano ya hadhara na matumizi ya teknolojia ya habari. Teknolojia hiyo imesaidia katika kurusha matangazo ya vikao vya Bunge moja kwa moja, jambo ambalo limeongeza uwazi na ushiriki wa wananchi katika masuala ya kitaifa," alisema.

### Mafanikio ya Bunge katika kipindi cha Miaka 100

Alisema kufikia kipindi cha Bunge la Kumi na Tatu (13), mafanikio mbalimbali yamepatikana ikiwemo kuongezeka kwa wigo wa uwakilishi na demokrasia Bungeni na kuimarika kwa shughuli za Kamati za Bunge katika kusimamia utekelezaji wa shughuli za Serikali

Alisema katika Miaka 100 ya Bunge, Tanzania imeshuhudia kuimarika kwa demokrasia na maendeleo ya Taifa, uwajibikaji wa Serikali mbele ya Bunge pamoja na ushiriki wa vijana, wanawake na watu wenye ulemavu katika siasa na shughuli za Kibunge.

"Katika kipindi hiki cha karne moja, Bunge limeendelea kuwa nguzo muhimu ya demokrasia, utungaji wa sheria, uwakilishi wa wananchi na usimamizi wa Serikali," alisema.





> **"Katika kipindi hiki cha karne moja, Bunge limeendelea kuwa nguzo muhimu ya demokrasia, utungaji wa sheria, uwakilishi wa wananchi na usimamizi wa Serikali," alisema.**

Aliyataja mafaniko mengine kwamba ni kuongezeka kwa matumizi ya mifumo ya kidijitali katika shughuli za Kibunge, kuimarika kwa diplomasia ya Kibunge kupitia ushiriki wa Tanzania katika mikutano mbalimbali ya Kikanda na Kimataifa, kuongezeka kwa uwazi katika shughuli za Bunge na kuendelea kwa maboresho ya miundombinu na mazingira.

Alisema mafanikio hayo yamechangia kuimarisha hadhi ya Bunge na kuongeza tija ya majukumu ya Bunge kwa wananchi.

## Uwajibikaji wa Serikali Mbele ya Bunge

Mhe. Spika alisema Bunge la Tanzania limeendelea kuimarika katika kutekeleza majukumu yake ya kuishauri na kuisimamia Serikali kwa kipindi chote cha historia.

Alisema kuimarika huko kumetokana na maboresho katika maeneo mbalimbali yakiwemo maswali ya Wabunge kwa Serikali, Kamati za Kudumu za Bunge, Kamati Teule, Kamati Maalum na uchambuzi na uidhinishaji wa bajeti.

Alisema maboresho mengine yaliyofanyika ni namna ya kushughulikia Taarifa za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), kuanzishwa kwa Maswali ya Papo kwa Papo kwa Waziri Mkuu, hoja za Wabunge na taarifa mbalimbali zinazowasilishwa na Serikali Bungeni.

"Maboresho haya yameendelea kuimarisha uwajibikaji, matumizi sahihi ya fedha za umma na utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa manufaa ya wananchi," alisema.

## Ushiriki wa Vijana, Wanawake na Watu wenye Ulemavu katika Siasa na Bungeni

Mhe. Spika alisema Bunge linaamini kuwa ushiriki wa wanawake, vijana na wenye ulemavu katika uongozi ni msingi muhimu wa demokrasia shirikishi.

Alisema Tanzania imeendelea kufanya vizuri katika uwakilishi wa makundi hayo Bungeni huku akitoa mfano kwamba takwimu zinaonesha kuwa uwakilishi wa wanawake katika Bunge umeendelea kuongezeka.



*Jarida la* Bunge | Toleo la Kumi na Tatu Septemba 2026

"Kwa sasa uwakilishi wa wanawake umefikia takribani asilimia 40, kiwango ambacho ni juu ya wastani wa dunia wa uwakilishi wa wanawake Bungeni ambao ni asilimia 27.5.

"Pia, katika Bunge la Tanzania kipo Chama cha Wabunge Wanawake Tanzania (TWPG) kilichoanzishwa mwaka 1993 kwa lengo la kuwajengea uwezo Wabunge Wanawake Bungeni," alisema.

Kwa upande wa uwakilishi wa Wabunge vijana katika Bunge, alisema uwakilishi wao umeendelea kuongezeka hadi kufikia Wabunge 72.

Alisema Wabunge vijana wameunda chama chao ambacho kimeanzishwa katika Bunge la 11 mwaka (2015–2020) kwa lengo la kuhamasisha Wabunge Vijana Bungeni.

"Vilevile uwakilishi wa wabunge wenye ulemavu umeendelea kuongezeka hasa kwa kuzingatia aina mbalimbali za ulemavu. Katika Bunge la Kumi na Tatu (13), idadi ya Wabunge wenye ulemavu wa aina tofauti imefikia wabunge 11," alisema.

Aidha, alisema Bunge linaendelea kushirikiana na taasisi mbalimbali katika kuhamasisha vijana kushiriki kikamilifu katika siasa, uongozi na michakato ya kidemokrasia kwa kutambua kuwa vijana ndiyo nguvu kazi ya Taifa.

## Mabadiliko mbalimbali

Awali akielezea chimbuko la Bunge la Tanzania alisema lilianza tarehe 19 Machi, 1926 wakati Tanganyika ikiwa chini ya utawala wa Waingereza.

"Siku hiyo Bunge la Uingereza lilipitisha Sheria iliyoitwa The Tanganyika *(Legislative Council) Order in Council, 1926*. Lengo la Sheria hiyo lilikuwa ni kuanzisha Baraza la Kutunga Sheria Tanganyika *(The Legislative Council of Tanganyika Territory – LEGCO),"* alisema.

Alisema Baraza hilo lilizinduliwa tarehe 10 Oktoba, 1926, Jijini Dar es Salaam katika ukumbi wa Shule ya Agakhan (Agakhan School) iliyokuwa inamilikiwa na Taasisi ya Agakhan ambayo kwa sasa ni Shule ya Sekondari Tambaza.

"Baada ya uzinduzi, kikao cha kwanza cha Baraza kilifanyika tarehe 07 Disemba, 1926 chini ya mwenyekiti wake Sir Donald Cameron aliyekuwa Gavana wa Tanganyika.

"Baraza la Kwanza liliundwa na Wajumbe 20 walioteuliwa na Gavana miongoni mwao wajumbe

> **Bunge la Uingereza lilipitisha Sheria iliyoitwa The Tanganyika (Legislative Council) Order in Council, 1926. Lengo la Sheria hiyo lilikuwa ni kuanzisha Baraza la Kutunga Sheria Tanganyika (The Legislative Council of Tanganyika Territory – LEGCO)**



*Jarida la* Bunge | Toleo la Kumi na Tatu Septemba 2026

wazungu walikuwa 19 na mhindi mmoja. Sheria zilizotungwa na Baraza zilikuwa zikipelekwa Uingereza ili kupata idhini ya Mfalme," alisema Mhe. Zungu.

Alisema historia inaonesha kuwa Bunge la Tanzania limepitia katika mabadiliko mbalimbali kuanzia kuundwa kwa Baraza la Kutunga Sheria Mwaka 1926 hadi sasa.

Alisema mabadiliko makubwa ya kwanza ni kuingia kwa watanganyika katika Baraza hilo mwaka 1945 ambao ni Chifu Abdieli Shangali aliyekuwa Chifu wa Wamachame kutoka Kilimanjaro na Chifu Kidaha Makwaia aliyekuwa Chifu wa Wasukuma kutoka Ukenyenge, Shinyanga.

"Mwaka 1947 aliongezeka Mtanganyika mwingine Bwana Juma Mwindadi na mwaka 1948 Chifu Adam Sapi Mkwawa aliteuliwa kuwa Mjumbe wa Baraza ambaye baadaye alikuja kuwa Spika wa Bunge kuanzia mwaka 1962 -1973, 1975 -1994," alisema

Mhe. Zungu alisema mabadiliko makubwa ya pili yalifanyika mwaka 1953, ambapo Gavana aliondolewa kuongoza Baraza na nafasi yake kuchukuliwa na Spika Brigedia William Erick Halstead Scupham aliyeapishwa tarehe 1 Novemba, 1953 na kwamba kwa wakati huo, Sheria zilizotungwa na Baraza la Kutunga Sheria zilianza kuidhinishwa na Gavana kwa niaba ya Malkia wa Uingereza.

"Mabadiliko makubwa ya tatu yalifanyika mwaka 1958, ambapo kwa mara ya kwanza Baraza lilipata wajumbe wa kuchaguliwa na wananchi kufuatia uchaguzi mdogo uliohusisha vyama vya *Tanganyika African National Union (TANU), United Tanganyika Party (UTP) na African National Congress (ANC).*

"Chama cha TANU kilishinda katika uchaguzi wa majimbo yote matano na hivyo kikawa chama pekee cha Waafrika chenye wajumbe katika Baraza la LEGCO, miongoni mwao alikuwepo Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, Baba wa Taifa," alisema.

Akizungumzia mabadiliko makubwa ya nne, alisema yalitokea mwaka 1960 ulipofanyika uchaguzi mkuu wa kwanza.







> **Mabadiliko ya mwaka 1964** ambapo Bunge lilikuwa na sura ya Muungano kwa kuwa na wabunge kutoka pande zote za Muungano, likiitwa Bunge la Tanganyika na Zanzibar ambalo liliongozwa na Spika Chifu Adam Sapi Mkwawa.

Alisema uchaguzi huo ulikuwa ni sehemu ya maandalizi ya Uhuru wa Tanganyika ambapo wajumbe wote wa Baraza walichaguliwa na kwamba jina la Baraza la Kutunga Sheria likabadilika kuwa Bunge.

"Lengo la mabadiliko hayo lilikuwa ni kuandaa mfumo wa kiutawala ili baada ya uhuru, Rais wa Tanganyika awe na mamlaka kikatiba ya kutoa idhini kwa sheria zilizotungwa na Bunge," alisema.

Mhe. Spika pia alizungumzia mabadiliko makubwa matatu yaliyofanyika baada ya uhuru mwaka 1961.

"Mosi, ni mabadiliko ya mwaka 1964 ambapo Bunge lilikuwa na sura ya Muungano kwa kuwa na Wabunge kutoka pande zote za Muungano, likiitwa Bunge la Tanganyika na Zanzibar ambalo liliongozwa na Spika Chifu Adam Sapi Mkwawa.

"Pili, ni mabadiliko ya mwaka 1965 yaliyohusisha marekebisho ya sheria yaliyolifanya Bunge kuwa la chama kimoja. Baada ya uchaguzi mkuu, liliundwa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

"Tatu, ni mabadiliko ya mwaka 1995 yaliyotokana na kurejeshwa kwa mfumo wa vyama vingi vya siasa nchini 1992. Baada ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 1995, Bunge likawa na wabunge kutoka vyama vingi vya siasa.

"Tangu wakati huo yameendelea kufanyika mabadiliko mengine madogo ya kimuundo na kimfumo yaliyojumuisha mabadiliko ya idadi na aina za wabunge," alisema Mhe. Spika.

Mhe. Spika alihitimisha kwa kuwaomba watanzania wote kuungana katika kuadhimisha miaka 100 ya Bunge.

"Niwahakikishie kuwa, Bunge tumejidhatiti katika kuendelea kusimamia ustawi wa wananchi kwa kuimarisha utendaji kazi wa Bunge," alisema.

Alisema kuadhimisha Miaka 100 ya Chimbuko la Bunge la Tanzania, hakuishii kusherehekea urithi wa Bunge pekee bali pia yatathibitisha kujitolea katika kujenga mustakabali imara, jumuishi zaidi na wa kidemokrasia.

Aliwahakikishia Watanzania kwamba Bunge litaendelea kutekeleza wajibu wake kwa weledi na uwazi ili kuwaletea wananchi maendeleo na pia kuzingatia maslahi ya Taifa.



# Waziri Mkuu Akemea Usumbufu Kwa Wajasiriamali

*Na Lawrence Raphaely*

Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Mwigulu Nchemba amesema vitendo vya baadhi ya watendaji wa mamlaka za udhibiti na usimamizi wa sheria kunyang'anya bidhaa, mitaji na vitendea kazi vya wajasiriamali mbalimbali katika maeneo mengi nchini havikubaliki na vinarudisha nyuma jitihada za wananchi kujikwamua kiuchumi.

Mhe. Dkt. Mwigulu aliyasema hayo tarehe 26 Juni, 2026 wakati akitoa Hotuba ya Kuhitimisha Mkutano wa Tatu wa Bunge la 13 ambao ulikuwa mahsusi kwa ajili ya kupokea na kujadili Bajeti ya Serikali.

Alisisitiza watendaji kuheshimu jasho la mtanzania, ikiwa ni pamoja na mitaji na shughuli zinazofanywa na wajasiriamali kote nchini.

"Dosari zozote zinazojitokeza katika shughuli zao zishughulikiwe kwa kutumia njia zisizohusisha kukamata mali na mitaji yao isipokuwa kwa makosa ya kijinai na yanayohatarisha usalama," alisema.

"Kama msimamizi wa shughuli za kiserikali nitaendelea kuchukua hatua kali ili kukomesha tabia hii," alisisitiza.





Aidha alisema Serikali imefanya maboresho katika sheria 55 pamoja kupunguza au kufuta tozo na ada 374 kwa lengo la kupunguza gharama za kufanya biashara, kuimarisha mazingira ya uwekezaji pamoja na kuongeza usajili wa biashara na uwekezaji nchini.

Alisema pamoja na maboresho hayo, lakini pia Serikali kwa kuzingatia maoni ya Waheshimiwa Wabunge kuhusu kero ya wingi wa ada na tozo katika ufanyaji biashara na uwekezaji, imedhamiria kuanzisha mfumo jumuishi ili kutatua kero hizo bila kuathiri majukumu ya msingi yanayofanywa na taasisi za udhibiti.

Vilevile, alisema hatua nyingine itakayochukuliwa ili kuwasaidia wajasiriamali, ni msamaha wa kodi ya mapato kwa wafanyabiashara wadogo ambao ni wapya kwa kipindi cha mwaka mmoja tangu tarehe ya kupata namba ya utambulisho wa mlipakodi.

"Hatua hii itawezesha mama na baba lishe, waendesha bodaboda na bajaji, mafundi seremala na wachomeleaji na wengine wenye shughuli ndogondogo kuanzisha biashara zao pasipo kuwepo changamoto ya kudaiwa kodi ndani ya mwaka mmoja, muda huo unatoa fursa ya kujiimarisha katika biashara wanazozianzisha," alisema.

Kuhusu malengo ya bajeti ya mwaka 2026/2027 alisema itasaidia katika kuweka mazingira wezeshi ya kuvutia urasimishaji wa sekta isiyo rasmi ambayo inaajiri zaidi vijana na wanawake.

Alisema katika kutekeleza azma hiyo, Serikali kupitia Mamlaka za Serikali za Mitaa itatenga asilimia 15 ya mapato yao ya ndani badala ya asilimia 10 iliyopo sasa ya mikopo ya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu.

"Kati ya asilimia 15 itakayotengwa, asilimia 10 itaelekezwa kwenye mikopo ya wanawake, vijana na wenye ulemavu kwa uwiano kama ilivyokuwa awali," alisema.

Pia alisema asilimia tano itatumika kwa ajili ya uwekezaji kwenye miradi ya ujenzi na maboresho ya masoko na maeneo ya biashara na ujasiriamali ili kuvutia na kuongeza fursa za ajira hususan kwa vijana, wanawake na makundi maalum.

"Nizielekeze Mamlaka za Serikali za Mitaa kutenga maeneo ya wajasiriamali kwa kuzingatia urahisi wa kufikika na kuwezesha kufanya biashara kwa tija," alisisitiza.



Kuhusu uimarishaji wa sekta za uzalishaji ikiwa nia pamoja na sekta ya kilimo alisema Serikali imeweka vivutio mbalimbali vya kikodi ili kuhamasisha kilimo na matumizi ya mbegu za mafuta zinazozalishwa nchini.

"Nafuu hii ni pamoja na kuhakikisha upatikanaji wa bidhaa hii kwa gharama nafuu na kulinda viwanda vya ndani vinavyochakata na kuzalisha mafuta ya kula yanayotokana na michikichi, soya, karanga pamoja na nazi," alisema.

Aliongeza kuwa Serikali itaendelea kuhakikisha viwanda vya ndani vinazalisha na kuwa shindani dhidi ya bidhaa zinazoingizwa nchini.

"Hatua hiyo, ni sehemu ya kuongeza kiwango cha ushuru wa forodha kwenye bidhaa mbalimbali zinazoagizwa kutoka nje ya nchi kwa lengo la kulinda viwanda vya ndani na kuhamasisha uwekezaji nchini," alisema.

Alisema katika mwaka wa fedha wa 2026/27 Serikali itatoa fedha zaidi kwa baadhi ya sekta za kimkakati ili kuziwezesha kukamilisha miundombinu na kurahisisha upatikanaji wa huduma muhimu karibu na maeneo ya wananchi.

"Lengo ni kukamilisha miundombinu ya reli ya SGR, ujenzi wa barabara, upanuzi wa Bandari ya Dar es Salaam na viwanja vingine," alisema.

Sambamba na hayo alisema katika sekta ya madini, Serikali imetenga fedha za kuweka mazingira wezeshi kwenye ujenzi wa viwanda vya kusafisha dhahabu, nickel, graphite, uranium na uboreshaji wa ramani za kina za madini nchini.

Kwa upande mwingine, Waziri Mkuu alizungumzia utatuzi wa kero za wananchi ambapo alisema ziara za viongozi wa kitafa katika maeneo mbalimbali nchini ni sehemu ya majukumu ya ufuatiliaji wa utekelezaji wa shughuli za Serikali ikiwemo utoaji wa huduma bora kwa wananchi.

Alisema katika ziara hizo wananchi wengi wamekuwa wanajitokeza kuwasilisha kero mbalimbali ambapo baadhi ya kero hizo, ilitarajiwa ziwe zimetatuliwa na viongozi waliopo kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa

"Ninawakumbusha viongozi na watumishi wote wa umma kwamba utatuzi wa kero za wananchi ni sehemu ya majukumu yao ya kila siku," alisema.

Aidha alielekeza Wizara, Idara, Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa kuhakikisha mifumo iliyopo kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa kuanzia ngazi ya mtaa/kijiji inatoa huduma kwa wananchi ipasavyo.

Pia alitaka Viongozi waendelee kutekeleza majukumu yao badala kusubiri teuzi.

Alisema suala la uteuzi halipaswi kuathiri utendaji kazi na dhamana ambazo zimetolewa na mamlaka ya uteuzi.

"Mamlaka inaendelea kufanya tathmini na wote wasiotimiza wajibu wao ipasavyo ikiwemo kuwahudumia wananchi watachukuliwa hatua," alisisitiza.

Mbali na hayo, Waziri Mkuu aliielekeza pia Wizara ya Fedha kwa kushirikiana na Wizara ya Maliasili na Utalii kuhakikisha wanawarejeshea wafugaji mifugo yao walioshinda kesi mahakamani.

Dkt. Mwigulu alisema kuwa baadhi ya wafugaji katika maeneo mbalimbali walitaifishiwa mifugo yao baada ya kukamatwa katika maeneo yaliyohifadhiwa.

"Tekelezeni maamuzi yaliyotolewa na mahakama kwa kuwarejeshea mifugo yao wafugaji walioshinda kesi mahakamani. Na kama mifugo hiyo ilikufa au ilipotea, basi wawarejeshee fidia ya mifugo yao," alisisitiza.

Waziri Mkuu alisema kuwa mashauri hayo yalikwishahitimishwa katika vyombo vya kisheria, ambapo wafugaji walipata ushindi na kuamriwa kurejeshewa mifugo yao.

> **Tekelezeni maamuzi yaliyotolewa na mahakama kwa kuwarejeshea mifugo yao wafugaji walioshinda kesi mahakamani. Na kama mifugo hiyo ilikufa au ilipotea, basi wawarejeshee fidia ya mifugo yao**
>
> **Waziri Mkuu, Mhe. Dkt Mwigulu Nchemba**





"Mpaka sasa taasisi husika hazijatekeleza maamuzi hayo ya mahakama. Badala yake wameishia kuwaambia wafugaji kuwa mifugo yao ilikufa, ilipotea au kutoa sababu nyingine. Vitendo hivyo vinadhoofisha sekta ya mifugo na kuwaacha wananchi hawa katika ufukara," alisema.

Katika hatua nyingine, akizungumza kuhusu migongano kwenye usimamizi wa shughuli katika Mamlaka za Serikali za Mitaa, Waziri Mkuu alisema kila mwaka Serikali inaingia gharama za uchaguzi ambapo viongozi na watendaji wanakuwa katika mchakato wa uchaguzi.

Alisema mazingira hayo yanazorotesha utendaji, yanachochea migongano na kuondoa utulivu kwenye mamlaka za Serikali za Mitaa na hivyo yatafanyika mabadiliko ya kuondoa chaguzi hizo.

"Katika mkutano ujao, Serikali itawasilisha mapendekezo ya marekebisho ya sheria kuhusu nafasi za Naibu Meya na Makamu Mwenyekiti wa Halmashauri. Tutaondoa uchaguzi kufanyika kila mwaka.

Lengo ni kubadilisha mfumo wa sasa na kuwa na Naibu Meya na Makamu Mwenyekiti kuwa kiongozi kwa kipindi chote cha uhai wa Baraza la Madiwani.

Marekebisho hayo yanatarajia kuleta utulivu, ili viongozi wajikite katika kufanya kazi na kujiekeleza kwenye shughuli za maendeleo ya wananchi katika maeneo yao," alisema.

Alisema ili kuimarisha misingi ya utawala wa kisheria na utoaji haki kwa wananchi, kupitia Mkutano wa Nne wa Bunge, Serikali itawasilisha mapendekezo ya marekebisho ya sheria zinazosimamia utaifishaji mifugo na mali kwenye maeneo yaliyohifadhiwa na itaenda kufutwa.

Mhe. Waziri Mkuu aliwakumbusha pia watendaji wa Serikali kuhakikisha wanatumia fedha za maendeleo wanazopelekewa kukamilisha miradi iliyokusudiwa kwa kuzingatia thamani ya fedha.

"Wakumbuke kuwa dhamira na maelekezo ya Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni kutekeleza kikamilifu miradi ya maendeleo kwa ajili ya ustawi wa Watanzania. Serikali itachukua hatua kwa watendaji wote ambao watashindwa kutekeleza maelekezo hayo," alisema.

# Mkutano wa 55 wa CPA Kanda ya Afrika

## Mabunge yaweka msisitizo wa kurejesha imani ya wananchi




*Na Deonisius Simba*

Mabunge ya nchi wanachama wa Chama cha Mabunge ya Jumuiya ya Madola (CPA), Kanda ya Afrika yametakiwa kuchukua hatua za kuhakikisha wananchi wanajenga imani kwa mabunge.

Wito huo ulitolewa na Rais wa CPA Kanda ya Afrika na Spika wa Bunge la Malawi, Mhe. Sameer Gaffar Suleman wakati akifungua Mkutano wa 55 wa CPA Kanda ya Afrika uliofanyika Jijini Lilongwe, Malawi, tarehe 9 hadi 15 Agosti 2026.

Mkutano huo uliowakutanisha zaidi ya wajumbe 300 kutoka mabunge ya kitaifa na ya Serikali za Majimbo katika Kanda ya Afrika ulifanyika katika Ukumbi wa Mikutano wa Kimataifa wa Bingu (BICC).

Mhe. Suleman alizitaka nchi za Afrika kuchukua hatua katika kujenga upya imani ya wananchi kwa mabunge.

Alisisitiza kuwa demokrasia haiwezi kudumu kwa sababu tu mabunge yapo, bali inadumu pale wananchi wanapoamini taasisi hizo na kuona kuwa zinawakilisha maslahi yao.

Alisema upo umuhimu wa kuwepo uwazi, uwajibikaji na ushirikishwaji ili kuzuia kuendelea kupungua kwa imani ya wananchi kwa taasisi za kidemokrasia.

Alisema Mabunge yanapaswa kuwa mstari wa mbele katika kuhakikisha ukuaji wa uchumi unakuwa wa watu wote na kwamba Mabunge yawe tayari kukabiliana na changamoto zinazobadilika katika Bara la Afrika.

Kwa upande wake, Katibu wa Bunge la Malawi na Katibu wa Tawi la CPA Malawi, Ndugu Fiona Kalemba, aliwakaribisha wajumbe wa mkutano



*Jarida la* Bunge | Toleo la Kumi na Tatu Septemba 2026



huo Jijini Lilongwe huku akieleza kuwa kuandaa Mkutano wa CPA Afrika nchini Malawi ni heshima kubwa, lakini pia ni jukumu lenye matarajio makubwa.

Alisisitiza kwamba CPA Afrika imeendelea kuwa moja ya majukwaa ya muda mrefu na yenye umuhimu mkubwa katika kukuza ushirikiano na kubadilishana uzoefu kati ya mabunge.

Kwa mujibu wa Kalemba alisema kupitia programu na mikutano yake, CPA Afrika inaendelea kujenga umoja, kuimarisha uhusiano wa kitaasisi na kukuza misingi ya utawala bora na majukumu ya msingi ya mabunge.

Kwa upande wake, Katibu Mkuu wa CPA, Stephen Twigg ,akizungumza katika ufunguzi wa Mkutano huo, aliwasilisha salamu kwa niaba ya Mwenyekiti wa CPA *International* ambaye pia ni Mbunge za Bunge la Zambia, Dkt. Christopher Kalila pamoja na Sekretarieti ya CPA Makao Makuu.

Twigg alieleza kwamba katika kipindi ambacho ushirikiano wa kimataifa unakabiliwa na changamoto mbalimbali Mabunge yanaweza kuwa vichocheo vya ukuaji jumuishi.

Alisema kufanya hivyo kunaendana na malengo makuu ya CPA ambayo ni kuimarisha mabunge, kujenga uwezo wa Wabunge na watumishi wa mabunge kitaaluma na kukuza maadili ya Jumuiya ya Madola.

Awali kabla ya ufunguzi rasmi wa Mkutano huo, Kamati Tendaji ya CPA Kanda ya Afrika ilikutana katika kikao chake cha 91 ikiongozwa na Mwenyekiti wa Kamati hiyo ambaye pia ni Spika wa Bunge la The Gambia Mhe. Fabakary Tombong Jatta.

Katika kikao hicho, Jatta alieleza kuwa uhusiano wa jadi kati ya Serikali na wananchi katika Bara la Afrika unakabiliwa na changamoto, hivyo mabunge yana wajibu mkubwa wa kuwa chombo kikuu cha kuhakikisha ujumuishi na kukuza maendeleo.

Alisisitiza kuwa uhusiano kati ya Serikali na wananchi Barani Afrika unajaribiwa na kwamba Mabunge yanapaswa kuwa chombo kikuu cha ujumuishi na ukuaji.

### Warsha na Majadiliano

Wakiwa Jijini Lilongwe kushiriki Mkutano huo, Wajumbe walishiriki katika warsha na majadiliano kuhusu baadhi ya changamoto zinazoikabili Afrika na dunia kwa ujumla.

Miongoni mwa masuala yaliyojadiliwa ni amani na usalama, ukosefu wa ajira kwa vijana, usawa wa kijinsia, mabadiliko ya tabianchi, Akili mnemba (Artificial Intelligence), utawala wa kidijitali na ujumuishaji wa makundi mbalimbali katika jamii.

Moja ya mjadala ulihusu namna ya kujenga Mabunge jumuishi ambapo Mwenyekiti wa Chama cha Wanawake wa Mabunge ya Jumuiya

ya Madola (CWP) Kanda ya Afrika na Mbunge wa Bunge la Rwanda, Mhe. Ndangiza Madina alisisitiza umuhimu wa ushiriki wa wanawake, vijana, watu wenye ulemavu na makundi yaliyotengwa katika michakato ya utawala.

Alieleza kuwa utawala jumuishi si jambo la hiari, bali ni msingi wa uhalali wa kidemokrasia, maendeleo endelevu na amani ya kudumu.

**Ushiriki wa Bunge la Tanzania katika Mkutano**

Tanzania ilikuwa miongoni mwa matawi ya CPA kanda ya Afrika yaliyoshiriki katika Mkutano huo. Ushiriki wa Tanzania ulikuwa muhimu kwa kuwa Bunge la Tanzania ni mwenyeji wa Sekretarieti ya CPA Kanda ya Afrika.

Katibu wa CPA Kanda ya Afrika, Ndugu Baraka Leonard, ambaye pia ni Katibu wa Bunge la Tanzania, alishiriki katika shughuli za mkutano huo.

Kwa upande wake, Mjumbe CPA na Mbunge wa Bunge la Tanzania, Mhe. Rose Cyprian Tweve aliongoza mada kuhusu Usimamizi wa Kibunge katika Mikataba ya Biashara ya Bara la Afrika Kufanya Eneo Huru la Biashara Barani Afrika (AfCFTA) ilete tija kwa mwananchi wa Afrika.

Alisema kuwa soko kubwa la pamoja lenye walaji zaidi ya bilioni 1.4 haliwezi kufanikiwa kama nchi wanachama zitaendelea kuwa na vikwazo na kuleta urasimu mipakani.

"Mikataba ya kibiashara haipaswi kuishia kwenye makaratasi na kumbi za mikutano pekee. Sauti na mahitaji ya wafanyabiashara wadogo, wakulima, na wazalishaji wa nchini lazima ziakisiwe katika sheria zetu za ndani," alisema Mhe. Tweve

Alainisha vipaumbele vinne vya kimkakati ambavyo Mabunge yanatakiwa kuvishughulikia haraka kwamba ni kuwainua wanawake na vijana, kuoanisha sheria za ndani, ushirikishwaji wa sekta binafsi na uwekezaji wa miundombinu.








Mhe. Tweve alihitimisha kwa kutoa rai kuwa, ufanisi wa AfCFTA utapimwa kwa kuangalia jinsi unavyopunguza umaskini na kuzalisha ajira mpya kwa vijana wa Afrika, na jukumu hilo liko mikononi mwa Wabunge kupitia mamlaka yao ya usimamizi wa bajeti na sera za Serikali.

Tukio hilo muhimu lilihudhuriwa na wajumbe wengine kutoka Bunge la Tanzania ambao ni Mhe. Bazilio Mbwilo, Mhe. Amina Said na Mhe. Asha Motto.

**CWP yaweka msisitizo katika uwakilishi wa wanawake**

Katika Mkutano huo, Chama cha Wanawake wa Mabunge ya Jumuiya ya Madola (CWP) Kanda ya Afrika pia kilifanya mkutano wake wa kibiashara.

Mkutano huo ulisimamia uchaguzi wa Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti wa CWP Kanda ya Afrika kwa kipindi cha mwaka 2026–2029 huku ukipokea




maombi rasmi ya matawi yaliyokuwa tayari kuandaa Warsha ya Kikanda ya Uhamasishaji wa Masuala ya Jinsia mwaka 2027.

Akifunga Mkutano huo, Rais wa CPA Kanda ya Afrika ambaye pia ni Spika wa Bunge la Malawi, Mhe. Sameer Gaffar Suleman aliyataka Mabunge wanachama kuhamisha mijadala kutoka kwenye majadiliano kwenda kwenye utekelezaji kwa kuimarisha taasisi za kibunge, usimamizi wa Serikali, kujenga uwezo na kuwawezesha zaidi wanawake na Wabunge vijana.

Alisema majadiliano na maazimio ya Mabunge yaliyotokana na Mkutano huo hayapaswi kubaki kwenye makaratasi.

Alisisitiza pia umuhimu wa ushirikiano na kujifunza kutoka kwa matawi mengine ya CPA, na kwamba mafanikio ya CPA yanapaswa kupimwa kwa mabadiliko ya vitendo yanayoonekana katika Mabunge na maisha ya wananchi.

Aliwashukuru washiriki kwa mchango wao katika kufanikisha Mkutano na kusema ushiriki wao umeimarisha mshikamano unaoendelea kuitambulisha CPA Kanda ya Afrika.

Mkutano wa 55 wa CPA Kanda ya Afrika uliwakutanisha Maspika, Naibu Maspika, Wabunge, Makatibu wa Mabunge, watendaji wa mabunge pamoja na waangalizi kutoka matawi mbalimbali ya CPA Afrika

Mkutano huo uliendeshwa chini ya kaulimbiu "Kuhuisha Mkataba wa Kijamii: Mabunge Kama Chocheo la Ukuaji Jumuishi na Imani ya Wananchi" huku mjadala mkuu ukijikita katika nafasi ya Mabunge katika kujenga maendeleo jumuishi, kuimarisha demokrasia na kurejesha imani ya wananchi kwa taasisi zao za uwakilishi.




# Spika Ashiriki Mkutano Jukwaa la Kibunge - Marekani

## Aleeza Hatua Za Tanzania Kukabiliana Na Mabadiliko Ya Tabianchi

*Na Said Mussa*

Spika wa Bunge Mhe. Mussa Azzan Zungu (Mb) amesema Bunge la Tanzania limechukua hatua madhubuti za kuhimiza matumizi ya nishati safi ikiwemo magari ya umeme na yanayotumia gesi.

Amesema hatua hizo zimelenga kuimarisha utekelezaji wa mipango ya kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi ili kufikia Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs).

Mhe. Spika aliyasema hayo Julai 14, 2026 wakati akiwasilisha Taarifa ya Bunge la Tanzania kuhusu matumizi ya nishati safi kwenye Jukwaa la Kibunge katika Mkutano wa Ngazi ya Juu wa Umoja wa Mataifa kuhusu Malengo ya Maendeleo Endelevu (HLPF) 2026.

Mkutano huo umefanyika katika Makao Makuu ya Umoja wa Mataifa (UN), Jijini New York, nchini Marekani.

Amesema Bunge la Tanzania limepitisha marekebisho ya sera na sheria za kodi yaliyopunguza ushuru wa magari ya umeme kutoka asilimia 25 hadi asilimia 10 na kwamba misamaha mbalimbali ya ushuru na kodi kwa baadhi ya magari yanayotumia umeme na gesi imetolewa ili kuongeza matumizi ya usafiri rafiki kwa mazingira.

"Hatua hizi zinalenga kuwahamasisha wananchi kutumia magari ya umeme na yanayotumia gesi, kupunguza uzalishaji wa hewa ya ukaa, kupunguza utegemezi wa uagizaji wa mafuta ya petroli kutoka nje ya nchi na kulinda mazingira," alisema Mhe. Zungu





> **Ninawakaribisha nyote Tanzania kushiriki Mkutano wa 153 wa IPU Jijini Arusha.** Hakuna changamoto za kiafya zinazopaswa kuwapa wasiwasi wageni wanaokuja Afrika Mashariki, hususan Tanzania, karibuni mfurahie Mlima Kilimanjaro na visiwa vya marashi ya karafuu, Zanzibar, - Mhe. Mussa Azzan Zungu.













Aidha, alisema Tanzania imeendelea kuimarisha mifumo ya kitaasisi ya kushughulikia masuala ya mazingira na mabadiliko ya tabianchi kwa kuanzisha vitengo maalumu vya usimamizi wa masuala hayo, kuimarisha uhifadhi wa vyanzo vya maji na kuweka mfumo wa kitaifa wa ufuatiliaji wa kaboni.

"Hatua hizi zinaonesha dhamira ya Tanzania ya kujenga uchumi unaozingatia maendeleo endelevu huku ikichangia juhudi za dunia za kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi," amesema.

Katika hatua nyingine, Mhe. Zungu alizialika Jumuiya za Kimataifa kushiriki Mkutano wa 153 wa Umoja wa Mabunge Duniani (IPU) utakaofanyika Jijini Arusha, akisisitiza kuwa Tanzania ni nchi salama na ipo tayari kuwakaribisha wajumbe kutoka mataifa mbalimbali.


"Ninawakaribisha nyote Tanzania kushiriki Mkutano wa 153 wa IPU Jijini Arusha. Hakuna changamoto za kiafya zinazopaswa kuwapa wasiwasi wageni wanaokuja Afrika Mashariki, hususan Tanzania, karibuni mfurahie Mlima Kilimanjaro na visiwa vya



marashi ya karafuu, Zanzibar," alisema Mhe. Zungu.

Mkutano huo pia ulihudhuriwa na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti, Mhe. Mashimba Ndaki pamoja na Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Afya na Masuala ya UKIMWI, Mhe. Zeyana Abdallah Hamid.

# Bunge Lapitisha Miswada Mitano ya Sheria



Na *Pius Myanda*

**Bunge limepitisha Miswada ya Sheria mitano katika Mkutano wake wa Nne uliofanyika Agosti 26 hadi Septemba 4, 2026, jijini Dodoma.**

Miswada hiyo mitatu ilisomwa Mara ya Kwanza katika Mkutano wa Tatu wa Bunge na Miswada miwili ilisomwa Mara ya Kwanza katika Mkutano wa Pili Bunge Jijini Dodoma.

Miswada hiyo ni Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali wa Mwaka 2026, Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na. 02) wa Mwaka 2026, Muswada wa Sheria wa Marekebisho ya Sheria za Kilimo wa Mwaka 2026, Muswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Tasnia ya Pareto wa Mwaka 2026 na Muswada wa Sheria ya Mikopo kwa Dhamana za Mali zinazohamishika wa Mwaka 2026.

Kwa mujibu wa Kanuni za Kudumu za Bunge, Muswada ukishasomwa mara ya kwanza Bungeni, Spika huuelekeza katika Kamati inayohusika kwa ajili ya kuufanyia uchambuzi.



Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali wa Mwaka 2026 na Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na. 02) wa Mwaka 2026 ilielekezwa kwa Kamati yaKudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria.

Kwa upande wa Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria za Kilimo wa Mwaka 2026, wenyewe ulielekezwa kwa Kamati ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo. Muswada huo unalenga kuboresha kanuni, usimamizi na maendeleo ya sekta ya kilimo.

Muswada mwingine ni Muswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Tasnia ya Pareto wa Mwaka 2026 ambao pia ulipelekwa katika Kamati ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo.





> **Kanuni ya 100 (2) ya** Kanuni za Kudumu za Bunge inaeleza kwamba Kamati iliyopelekewa Muswada itatoa matangazo au itatoa barua ya mwaliko kumwalika mtu yeyote afike kutoa maoni yake mbele ya Kamati.

*Jarida la* Bunge | Toleo la Kumi na Tatu Septemba 2026

Muswada huo unalenga kufuta Sheria ya Tasnia ya Pareto na kuweka masharti kuhusu uhamisho wa mali, madeni na watumishi wa Bodi ya Pareto pamoja na kuweka masharti ya mpito na masuala mengine yanayohusiana na hayo.

Kwa upande wa Muswada wa Sheria ya Mikopo kwa Dhamana za Mali zinazohamishika wa Mwaka 2026 ulipelekwa Kamati ya Bunge ya Bajeti kwa ajili ya kufanyiwa uchambuzi.

Katika mchakato wa Bunge kutimiza majukumu yake ya utungaji wa sheria, miswada mbalimbali ya sheria baada ya kutangazwa katika Gazeti la Serikali huwasilishwa Bungeni na kusomwa Mara ya Kwanza.

Hatua hii hutekelezwa kwa mujibu wa Kanuni ya 99 (1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge.

Muswada husomwa Mara ya Kwanza Bungeni ikiwa na mantiki ya kuuweka wazi kwa kila mtu na pia hutoa fursa kwa umma kutoa maoni yao kupitia Kamati za Kudumu za Bunge.

Muswada hupelekwa katika Kamati ya Bunge kwa mujibu wa Kanuni ya 100 (1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Bunge.

Kamati zilizopelekewa miswada zilifanya vikao na kuchambua miswada hiyo pamoja na kukutana na wadau mbalimbali waliojitokeza kutoa michango yao juu ya miswada ya sheria hizo.

Ushirikishwaji wa wadau ni muhimu kwa kuwa baadhi ya mabadiliko yanayopendekezwa yanaweza kuwa na athari za moja kwa moja kwa watu, taasisi au sekta zinazohusika na sheria hizo.

Kanuni ya 100 (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge inaeleza kwamba Kamati iliyopelekewa Muswada itatoa matangazo au itatoa barua ya mwaliko kumwalika mtu yeyote afike kutoa maoni yake mbele ya Kamati.

Lengo ni kuisaidia Kamati katika uchambuzi wa muswada huo na baadae Kamati kutoa marekebisho yake kwa kumshauri Waziri anaye husika na muswada huo.

Baada ya Kamati kukamilisha kazi ya kuchambua muswada, humtaarifu Spika kwa ajili ya kuendelea na hatua nyingine ambazo ni Kusomwa Mara ya Pili na Kusomwa Mara ya Tatu na baadaye muswada utapata kibali cha Rais ili kuwa Sheria.




# “Tanzania Inatekeleza Kwa Ufanisi Ajenda 2063 Ya AU”

*Naibu Spika Sillo*

*Na Zuhura Mtatifikolo*

**Naibu Spika wa Bunge la Tanzania, Mhe. Daniel Baran Sillo, amesema Tanzania ni miongoni mwa nchi zinazotekeleza kwa ufanisi Ajenda 2063 ya Umoja wa Afrika.**

Mhe. Sillo alisema hayo wakati akichangia mjadala wa uzoefu wa nchi katika utekelezaji wa Ajenda 2063 katika Mkutano wa Maspika wa Mabunge ya Kitaifa na Kikanda ya Afrika uliofanyika Mjini Midrand, Afrika Kusini.

Naibu Spika alishiriki katika Mkutano huo kwa niaba ya Spika wa Bunge, Mhe. Mussa Azzan Zungu.

Akieleza uzoefu wa Tanzania, Mhe. Sillo alisema nchi imefanikiwa kujumuisha malengo ya Ajenda 2063 katika Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050.





**“Tanzania imeridhia na inatekeleza Mkataba wa African Continental Free Trade Area - AfCFTA, inashirikisha wananchi na Sekta Binafsi katika utekelezaji wa Ajenda 2063. Vilevile, Tanzania imekuwa ikifanya ufuatiliaji na tathmini katika utekelezaji wa Ajenda hiyo.”**

Naibu Spika Mhe.Daniel Baran Sillo

“Tanzania imeridhia na inatekeleza Mkataba wa African Continental Free Trade Area - AfCFTA, inashirikisha wananchi na sekta binafsi katika utekelezaji wa Ajenda 2063. Vileile, Tanzania imekuwa ikifanya ufuatiliaji na tathmini katika utekelezaji wa Ajenda hiyo” alisema.

Mhe. Sillo alieleza namna Bunge la Tanzania linavyoshiriki katika utekelezaji wa Ajenda 2063 kwa kutenga na kuidhinisha bajeti ya imkakati na utekelezaji wa miradi muhimu ya kikanda.

“Miradi hiyo ni pamoja na ujenzi wa One Border Post, barabara za kikanda, viwanja vya ndege, ujenzi wa reli pamoja na miundombinu mingine ambayo inachochea ukuaji wa ushirikiano wa kiuchumi katika jumuiya za kikanda” alisema.

Aliongeza kuwa Bunge pia linashiriki kikamilifu katika utekelezaji wa diplomasia ya kibunge, kuishauri na kuisimamia Serikali katika utekelezaji wa Ajenda 2063.

Katika hatua nyingine, Mhe. Sillo ameteuliwa kuwa Mwakilishi wa Kanda ya Mashariki mwa Afrika katika Uongozi wa Mkutano wa Maspika *(Bureau of the Conference)*

Uteuzi huo unatoa fursa kwa Tanzania kuongoza mijadala na maamuzi ya masuala ya Mabunge katika Bara la Afrika kwa kipindi cha mwaka mmoja.



# LAAC na PAC zahoji Wizara, Taasisi *na* Halmashauri Matumizi ya Fedha

*Na Brian Lugusha*

Kamati za Kudumu za Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC) na Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa (LAAC) zilikutana tarehe 3 hadi 21 Agosti Jijini Dodoma kabla ya kuanza kwa Mkutano wa Nne wa Bunge.

Kamati hizo zilichambua Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kuhusu hesabu za Wizara, Taasisi mbalimbali za Umma, Mashirika ya Umma na Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa Mwaka wa Fedha unaoishia Juni 30, 2025 zilizokaguliwa.

Lengo ni kuhakiki matumizi sahihi ya fedha za umma kwa kuzingatia utaratibu uliowekwa kwa mujibu wa fasili ya 13 na 14 ya Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Bunge za Mwaka 2025.

Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa (LAAC) inayongozwa na Mwenyekiti wake Mhe. Ado Shaibu Ado ilihoji na kuchambua taarifa zinazohusu hesabu za Halmashauri 39 nchini kufuatia Ripoti ya CAG.

Baadhi ya halmashauri zilizohojiwa na Kamati hiyo ni pamoja na Halmashauri ya Manispaa ya Singida, Halmashauri ya Mji Kasulu, Halmashauri ya Wilaya ya Uvinza, Halmashauri ya Wilaya ya Sikonge, Halmashauri ya wilaya ya Bagamoyo na Halmashauri ya Manispaa ya Ubungo.

Nyingine ni Halmashauri ya Manispaa ya Shinyanga, Halmashauri ya Wilaya ya Bukombe, Halmashauri ya Manispaa ya Musoma, Halmashauri ya Mji Babati, Halmashauri ya Wilaya ya Moshi na Halmashauri ya

> **Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa (LAAC) inayongozwa na Mwenyekiti wake** Mhe. Ado Shaibu Ado ilihoji na kuchambua taarifa zinazohusu hesabu za Halmashauri 39 nchini kufuatia Ripoti ya CAG





> PAC ilipitia na kuchambua Ripoti kuhusu hesabu za Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Wizara ya Ujenzi, Wizara ya Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Wizara ya Habari Utamaduni na Michezo, Wizara ya Maji pamoja na Ofisi ya Rais Mipango na

Wilaya ya Tarime.

Mijadala katika LAAC ilijikita katika maeneo mbalimbali baadhi ikiwa ni uboreshaji wa ukusanyaji wa ndani wa mapato ya halmashauri ili ziweze kujitegemea na kupunguza mzigo kwa Serikali.

Vilevile, Halmashauri zilitakiwa kuwa na tabia ya kufanya uwekezaji kwenye miradi mbalimbali katika maeneo yao ili kupata mapato yatakayowezesha shughuli za kimaendeleo badala ya kutegemea moja kwa moja fedha kutoka Serikali Kuu.

LAAC pia ilipitia taarifa za utekelezaji wa hoja na maelekezo yaliyotolewa na CAG kwenye halmashauri zinazohusika.

PAC inayongozwa na Mwenyekiti Mhe. Devota Minja, ilipitia Ripoti za Hesabu zilizokaguliwa na CAG kwa mafungu ya Wizara saba, Taasisi za Umma 15, Wakala sita pamoja na Mifuko minne.

PAC ilipitia na kuchambua Ripoti kuhusu hesabu za Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Wizara ya Ujenzi, Wizara ya Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Wizara ya Habari Utamaduni na Michezo, Wizara ya Maji pamoja na Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji.

Aidha, Kamati hiyo ilifanikiwa kufanya mapitio na kuchambua Taarifa ya Mifuko mbalimbali ya Taifa kama vile Mfuko wa Taifa wa Maji, Mfuko wa Utamaduni na Sanaa, Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma (PSSSF).

Kwa upande wa baadhi ya Mashirika ya Umma yaliyofika mbele ya PAC ni Shirika la Nyumba la Taifa (NHC) Kampuni ya Ndege ya Tanzania (ATCL), Shirika la Hifadhi ya Taifa Tanzania (TANAPA) na Shirika la Umeme Tanzania.

PAC ilipitia Taarifa za hesabu za Taasisi mbalimbali za Umma ikiwemo Bohari Kuu ya Dawa (MSD), Mamlaka ya Udhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya, Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi (VETA), Chuo Kikuu cha Mzumbe, Wakala wa Mabasi Yaendayo Haraka (DART), Kampuni ya





Mbolea Tanzania (TCP) na Wakala wa Ufundi na Umeme (TEMESA).

Kamati hiyo ilibaini dosari mbalimbali na kuzielekeza taasisi za umma zizingatie taratibu za ununuzi wa umma, zifanyie kazi maelekezo mbalimbali ya Kamati na hoja za CAG.

*Jarida la* Bunge | Toleo la Kumi na Tatu Septemba 2026




# Ofisi ya Bunge yashiriki Maonesho Mbalimbali

Na Debora Sanja

Ofisi ya Bunge kama ilivyo ada imeshiriki maonesho mbalimbali kwa lengo la kutoa elimu kuhusu Bunge kwa wageni wanaotembelea maonesho hayo.

Katika kipindi cha hivi karibuni, Ofisi imeshiriki katika Maonesho ya Wiki ya Utumishi wa Umma yaliyofanyika Juni 17-23, 2026 Viwanja vya Chinangali Park jijini Dodoma ambayo yalibeba Kauli Mbiu ya "Kuchochea Uwajibikaji kwa Huduma Endelevu."

Maonesho mengine ambayo Ofisi ya Bunge ilishiriki ni Maonesho ya 50 ya Kibiashara ya Kimataifa (Sabasaba) yaliyofanyika Juni 28 hadi Julai 13, 2026 jijini Dar es Salaam.

Maonesho hayo yanayoandaliwa na Wizara ya Viwanda na Biashara kupitia Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania (TANTRADE) yalikuwa na Kauli Mbiu isemayo "Maonesho ya Kibiashara ya Kimataifa Sabasaba, Fahari ya Tanzania".

Maonesho mengine ni Maonesho ya 33 Kimataifa ya Kilimo (Nanenane) yaliyofanyika tarehe Agosti 1 hadi 8,2026 katika Uwanja wa Nanenane Nzuguni jijini Dodoma na yalibeba Kauli Mbiu ya"Tambua Soko, Ongeza Tija Kutekeleza Dira 2050.

Maafisa wa Bunge walitumia fursa hiyo ya maonesho kutoa elimu kuhusiana na Mhimili wa Bunge, muundo wake na majukumu yake.

Vilevile, waligawa machapisho mbalimbali ikiwemo majarida, Kanuni za Kudumu za Bunge, kitabu cha Lijue Bunge Lako na kitabu cha Historia ya Bunge tangu mwaka 1926 kwa wananchi waliofika katika mabanda ya Ofisi ya Bunge.

Vilevile, Ofisi ya Bunge ilibeba ujumbe maalumu kuhusiana na matukio makubwa yatakayofanyika ambayo ni Maadhimisho ya Miaka 100 ya Chimbuko la Bunge la Tanzania na Mkutano wa 153 wa Umoja wa Mabunge Duniani (IPU) unaotarajiwa kufanyika Oktoba mwaka huu jijini Arusha.

Mabanda ya Ofisi ya Bunge yalisheheni mabango mbalimbali yaliyoeleza matukio hayo mawili makubwa.

Maelfu ya wananchi walijitokeza kwa wingi kutembelea mabanda ya Ofisi ya Bunge na kupata fursa ya kujifunza na pia kujionea alama mbalimbali za Bunge ikiwemo Joho la Spika, Kiti cha Spika, mfano wa Siwa na nyaraka mbalimbali ikiwemo Hansard.

Aidha, viongozi mbalimbali walitembelea Banda la Bunge wakiwemo mawaziri, mabalozi, wakuu wa taasisi, wakuu wa vyombo vya ulinzi na usalama na Waheshimiwa Wabunge.

# Picha za Matukio Mbalimbali ya Saba Saba na Nane Nane











# Mfahamu Randhir Thaker na Uhusiano Wake na Bunge

*Na Abdallah S. Hancha,* ndc

**Katika hitimisho la toleo lilopita tulimwelezea Randhir Thaker, Mchapishaji, mhariri, na mwanzilishi wa gazeti la Tanganyika liitwalo Ngurumo (1921-1965) na uhusiano wake na Bunge.**

Ingawa hakuwa Mbunge, afisa wa Serikali, au afisa wa Bunge, mchango wake katika mageuzi ya kisiasa ya Tanganyika ulimuunganisha kwa karibu na viongozi, wawakilishi na taasisi ya Bunge. Hivyo katika toleo hili tunahitimisha uchambuzi kuhusu mchapishaji huyu na mhariri mahiri.

## Thaker na Mwl. Nyerere

Rais wa Kwanza wa Tanzania, Mwl. Nyerere alikuwa ni Rafiki mkubwa wa Ndg. Thaker. Mwalimu na marehemu walikuwa wakitembeleana na kuzungumza kwa muda mrefu mambo mbalimbali ya kijamii na kisiasa.

Kutokana na urafiki huo na harakati za Thaker kuisadia TANU na pia kuwa mstari wa mbele katika harakati za uhuru wa Tanganyika, siku ya mazishi yake Mwl. Nyerere alikuwepo.

Kama ilivyo desturi ya dini yao Bwana thaker alizikwa kwa kuchomwa moto Novemba, 1965. Wakati wa mazishi, Mwl. Nyerere alionekana akivuta tafakuri namna yeye na marehmu walivyokuwa wakisadiana kupeleka mbele gurudumu la maendeleo ya Tanganyika na baadaye Tanzania. Mwalimu alishindwa kujizuia kutoa machozi.

## Neno la Mhe. Waziri Bhoke Munanka

Aliyekuwa Waziri wa nchi katika Ofisi ya Rais wakati huo (1965), Bwana Bhoke Munanka aliongea maneno mazito kuhusu marehemu



Thaker. Akizungumza wakati wa kumuombea marehemu Thaker katika Ukumbi wa Maktaba ya T. B Seth, Munanka alitoa ombi kwa waasia wote wa Tanzania kuiga mfano wa kujitolea kwelikweli kama alivyokuwa anajitolea Bwana Randhir Thaker.

Alimsifu marehemu kuwa hakuwa na ubaguzi wa kabila, dini au rangi kwani alikuwa akiwasaidia watu binafsi kwa shida zao mbalimbali. Maneno ya Mhe. Munanka yanathibitishwa na mmoja wa washairi wa zama hizo K. M. Ramadhani alipotunga shairi kumlilia Ndg. Thaker na kuielezea tabia yake ilivyokuwa. Shairi hilo lenye beti saba liitwalo Rambirambi lilichapwa katika gazeti la Ngurumo Novemba 11, 1965.

**Rambi Rambi**

1. Tumejawa na huzuni, Mhariri katutoka,
   Pengo lisilo kifani, lisoweza kuzibika,
   Alitakalo Manani, daima hukamilika,
   Mola wetu muhifadhi, marehemu Bwana Thaker.

2. Twazikumbuka hisani, misaada kadhalika,
   Akuonapo fulani, na kitini hunyanyuka,
   Akujue watakani, na huku ashughulika,
   Mola wetu muhifadhi, marehemu Bwana Thaker.

3. Mfano wake nadhani, milele tutakumbuka,
   . Juhudi zake Chamani, nchini zatambulika,
   Fedha hakuithamini, heshima mbele kaweka,
   Mola wetu muhifadhi, marehemu Bwana Thaker.

4. Tajiri na masikini, tofauti hakutaka,
   Tarishi au karani, tabasamu na kucheka,
   Yaillahi Ya-Rubani, twaomba kwako Rabuka,
   Mola wetu muhifadhi, marehemu Bwana Thaker:

5. Katutoka duniani, ghafla hakuteseka,
   Jamaa na wa-kazini, sote tumefadhaika,
   Faradhi hii si deni, mbona lingalilipika,
   Mola wetu muhifadhi, marehemu Bwana Thaker.



*Jarida la Bunge* | Toleo la Kumi na Tatu Septemba 2026

> **Randhir Thaker hakuwa Mbunge, lakini ushawishi wake ulikuwa wa kiwango cha juu katika historia ya kisiasa na kisheria ya Tanzania.** *Kupitia uchapishaji na uandishi wa habari, alichangia ukuaji wa ufahamu wa kisiasa wakati wa kipindi muhimu cha mabadiliko ya katiba na uongozi wa nchi.*

6. Rais na usukani, mashtaka kumfika,
   Alikuwa namba wani, kortini kusumbuka,
   Siku zile Ukoloni, nyakati za hekaheka,
   Mola wetu muhifadhi, marehemu Bwana Thaker.

7. Wana na mama nyumbani, pamoja twaunganika
   Twasema wote poleni, ndivyo ilivyobidika,
   Huzaliwa utotoni, na mwisho ni kuondoka,
   Mola wetu muhifadhi, marehemu Bwana Thaker.

**K. M. Ramadhani (Chipukizi),**
**Ilala, Dar es Salaam.**
**Ngurumo, Novemba 11, 1965. Uk. 3**

## Historia fupi wa Thaker

Randhir B. Thaker alizaliwa Dar es Salaam mwaka wa 1921 katika familia yenye asili ya kihindi (Gujarati) iliyohusika katika masuala ya uchapishaji.

Alisomea Tanganyika na baadaye India, ambapo alihitimu kabla ya kurudi Tanganyika mwanzoni mwa miaka ya 1950.

Alianzisha Thakers Ltd. mwaka wa 1953, biashara ya uchapishaji na vifaa vya kuandikia (stationery) ambapo Ofisi hiyo ikawa kitovu cha uchapishaji na vuguvugu la kisisasa kwa kuwa taarifa nyingi za TANU zilichapwa na kufika kwa wananchi kirahisi. Mwaka 1959 alianzisha gazeti la Ngurumo, gazeti la kila siku la lugha ya Kiswahili. Gazeti hilo lilikuza na kuimarisha fikra za uzalendo na kuchangia ukuaji wa Kiswahili kama lugha ya taifa. Kifupi, gazeti la Ngurumo lilikuwa na ushawishi mkubwa kisiasa na kijamii hadi lilipoanguka na hatimaye kufungwa mwaka wa 1976.

Bwana Thaker alikuwa mwanachama wa Tume ya Serikali za Mitaa na pia alikuwa Katibu wa Mara *Youth Settlement*, ambao unasemwa ni mmoja wa mipango ambao ulikuwa wa aina ya kipekee kwa wakati ule.

Thaker akiwa ni mdau wa habari, alisaidia kutoa mafunzo kwa kizazi cha waandishi wa habari katika Tanzania baada ya ukoloni.

Thaker alifariki ghafla kutokana na mshtuko wa moyo tarehe 02 Novemba, 1965 jijini Dar es Salaam. Kifo chake kiliombolezwa sana, na hata Rais Nyerere alihudhuria mazishi yake, ishara iliyoonesha umuhimu wake kitaifa.

Randhir Thaker hakuwa Mbunge, lakini ushawishi wake ulikuwa wa kiwango cha juu katika historia ya kisiasa na kisheria ya Tanzania. Kupitia uchapishaji na uandishi wa habari, alichangia ukuaji wa ufahamu wa kisiasa wakati wa kipindi muhimu cha mabadiliko ya katiba na uongozi wa nchi.

Uungaji wake mkono siasa za uzalendo, uhusiano wake na mawasiliano ya umma na kuanzisha kwa Ngurumo kulimuunganisha kwa njia isiyo ya moja kwa moja lakini yenye maana na Baraza la Kutunga Sheria kisha Bunge la Tanganyika na baadaye Bunge la Muungano.

Katika historia ya Bunge, ni muhimu kutambua kwamba, umuhimu si wawakilishi waliochaguliwa tu bali pia wale wanaosaidia kuweka mazingira mazuri ya ushiriki wa kidemokrasia. Randhir Thaker ni miongoni mwa watu wenye ushawishi ambao kazi yao iliimarisha ushiriki wa umma, kuelimisha mijadala ya kisiasa, na kuunga mkono maendeleo ya utawala wa Bunge nchini Tanganyika.







# Ukuaji na Maendeleo ya Sekretarieti ya Bunge la Tanzania

*Na Abdallah S. Hancha*, ndc

## Utangulizi

Historia ya Sekretarieti ya Bunge nchini Tanzania, inaonesha safari ndefu ya mabadiliko katika taasisi hii ya kidemokrasia na utawala. Kwa kipindi cha miaka mia moja, Ofisi ya Bunge imebadilika kutoka chombo kidogo kilichotegemea watumishi wa Serikali hadi kuwa taasisi ambayo ni sekretarieti ya kitaalamu inayotoa huduma kwa Wabunge, Kamati na Uongozi wa Bunge. Ukuaji huo umechangiwa na mabadiliko ya kisiasa, kikatiba, kiutawala na kiteknolojia, pamoja na kuongezeka kwa majukumu ya Bunge.

Sekretarieti ya Bunge ni uti wa mgongo wa kiutawala na kiufundi wa shughuli za Bunge. Inahakikisha kuwa Wabunge wanapata huduma zinazowawezesha kutekeleza majukumu yao ya kutunga sheria, kuwakilisha wananchi na kuisimamia Serikali. Kwa hiyo, historia ya ukuaji wa Sekretariati haiwezi kutenganishwa na historia ya maendeleo ya Bunge lenyewe.

Makala haya yanaangazia safari ya Sekretarieti tangu kuanzishwa kwa Baraza la Kutunga Sheria mwaka 1926, kipindi cha baada ya Uhuru, kutambuliwa kwake kikatiba mwaka 1984, mageuzi ya mfumo wa vyama vingi, kuanzishwa kwa Tume ya Huduma za Bunge mwaka 1997, na mabadiliko ya muundo wa kitaasisi hadi mwaka 2024. Pia inaonesha ukuaji wa idadi ya watumishi kutoka mtumishi mmoja mwaka 1926 hadi watumishi 330 mwaka 2026.

## Ofisi ya Bunge kabla ya Uhuru

Kabla ya Uhuru wa Tanganyika, Bunge lilijulikana kama Baraza la Kutunga Sheria lililoanza mwaka 1926. Ofisi ya Baraza ilikuwa ndogo sana na shughuli zake nyingi zilitegemea watendaji wa Serikali ya kikoloni. Maafisa waliokuwa na majukumu ya kawaida serikalini waliweza kupewa kazi za kulihudumia Baraza wakati wa vikao na baadaye kurejea katika majukumu yao ya Serikali.

Mwaka 1926, Baraza la Kutunga Sheria lilikuwa na mtumishi mmoja tu, ambaye alikuwa Katibu wa Baraza. Hii inaonesha udogo wa sekretarieti katika hatua za mwanzo. Katibu alikuwa kiungo muhimu katika kuratibu shughuli za Baraza, kumbukumbu na mahitaji ya kiutawala.



Baada ya miaka kadhaa, mahitaji ya uendeshaji wa Baraza yaliongezeka. Mwaka 1953 baada ya Gavana kukoma kuwa mwenyekiti wa Baraza ka kuchaguliwa Spika, watumishi wakawa wawili, ambao ni Spika wa Baraza na Katibu wa Bunge. Hata hivyo, bado secretarieti ilikuwa mdogo na uliendelea kutegemea watumishi na rasilimali kutoka Serikalini.

Utaratibu wa kutegemea watumishi wa Serikali ulikuwa na faida ya kulipatia Bunge utaalamu uliokuwepo serikalini, lakini pia ulikuwa na changamoto. Bunge halikuwa na mamlaka juu ya ajira na maendeleo ya watumishi hao, huku baadhi ya maafisa wakiwa na uhusiano wa kiutumishi na taasisi zao za Serikali. Hali hii pia ilifanya kujenga kumbukumbu na utaalamu wa kudumu wa Bunge kuwa jambo gumu.

## Ofisi ya Bunge baada ya Uhuru

Baada ya Tanganyika kupata Uhuru mwaka 1961, na baadaye kuundwa kwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mwaka 1964, Ofisi ya Bunge iliendelea kwa kiasi kikubwa kutegemea maafisa waliotoka Serikalini. Ni idadi ndogo ya watumishi iliyokuwa ikifanya kazi moja kwa moja chini ya Bunge. Hili linathibitishwa na orodha ya watumishi (*Staff list)* ya mwaka 1957 ambayo inaonesha watumishi wa Baraza la Kutunga sheia walikuwa saba tu.

Maafisa wenye ujuzi wa utawala, sheria, uhazili na fani nyingine kutoka serikalini waliweza kutumwa kwa muda kusaidia shughuli za Bunge. Mfumo huu uliwezesha Bunge kupata wataalamu katika kipindi ambacho Sekretarieti yake ilikuwa bado inajengwa. Hata hivyo, kuazimwa kwa watumishi kutoka Serikali kwenda Bunge na kurejea kwao Serikalini baada ya kuahishwa Bunge kuliathiri mwendelezo wa kumbukumbu na utaalamu wa kitaasisi.

Kadiri majukumu ya Bunge yalivyoongezeka, hitaji la kuwa na watumishi wake wenye utaalamu maalumu lilizidi kuonekana. Bunge lilihitaji huduma za kudumu katika maeneo ya sheria, utafiti, maktaba, kamati, taarifa rasmi, utawala, fedha na huduma kwa Wabunge.

### Ofisi ya Bunge chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu

Katika miaka ya mwanzo baada ya Uhuru hadi miaka ya 1986, Bunge lilifanya kazi kwa kiasi kikubwa kama idara chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu. Muundo wa Ofisi ya Bunge ulikuwa na sehemu kuu



tatu zilizobeba shughuli zake: Sehemu ya Uchaguzi, Sehemu ya Shughuli za Bunge na Sehemu ya Uhasibu.

Sehemu ya Uchaguzi ilisimamia shughuli za uchaguzi na kutoa huduma kama Tume ya Uchaguzi ambayo kwa wakati huo Spika ndiye aliyekuwa Mwenyekiti wake na Katibu wa Bunge alikuwa ndiye Mkurugenzi wa Uchaguzi. Sehemu ya Shughuli za Bunge ilisimamia shughuli za utumishi, uendeshaji na kazi za Bunge. Sehemu ya Uhasibu ilisimamia fedha, malipo na masuala ya kifedha ya Ofisi ya Bunge na Tume ya Uchaguzi.

Mwaka 1987, muundo uliimarishwa kwa kuongeza sehemu kutoka tatu hadi saba. Sehemu hizo zilihusu Uchaguzi; Shughuli za Bunge; Utumishi na Uendeshaji; Maktaba; Ukatibu wa Fedha na Uchumi; Ukatibu wa Katiba na Sheria; na Ukatibu wa Uongozi na Siasa. Pia kulikuwa na Vitengo vya Ukaguzi wa Ndani na Fedha na Uhasibu.

Mabadiliko haya yalionesha kuwa mahitaji ya Bunge yalikuwa yanaongezeka. Ingawa bado halikuwa na kiwango cha uhuru wa kiutawala kama ilivyo sasa, hatua hiyo iliweka msingi wa kuanza kujenga muundo wa kitaalamu zaidi wa Ofisi ya Bunge.

### Kutambuliwa kwa Sekretarieti ya Bunge kikatiba, 1984

Hatua muhimu katika maendeleo ya kitaasisi ilitokea mwaka 1984 wakati Ofisi ya Bunge na Katibu wa Bunge walipotambuliwa rasmi kikatiba kufuatia Sheria ya Marekebisho ya Tano ya Katiba ya Nchi ya mwaka 1984 (Na. 15).Kwa mujibu wa marekebisho hayo ya Katiba, Ibara ya 87(1) ilitambua nafasi ya Katibu wa Bunge, wakati Ibara ya 88(2) ilitambua kuwepo kwa Sekretariat ya Bunge.

Utambuzi huu ulikuwa muhimu kwa sababu uliimarisha hadhi ya kisheria na kiutawala ya Bunge. Katibu wa Bunge akawa mtendaji mkuu muhimu katika kusimamia shughuli za Ofisi ya Bunge, kuratibu huduma kwa Bunge na kuhakikisha kuwa shughuli za kila siku zinaendeshwa kwa ufanisi.

Katiba pia iliweka msingi wa kuamua idadi na ngazi za watumishi wa Sekretarieti kwa mujibu wa mahitaji ya taasisi. Hivyo, hatua ya mwaka 1984 ilikuwa msingi muhimu wa mageuzi yaliyofuata kuelekea Sekretariat yenye watumishi na muundo unaojitegemea zaidi.

> **Baada ya kuanzishwa kwa Tume mwaka 1997, muundo mpya wa Ofisi ya Bunge uliundwa.** Kwa mara ya kwanza kukawa na Idara nne: Idara ya Kamati za Bunge; Idara ya Shughuli za Bunge; Idara ya Maktaba na Utafiti; na Idara ya Utawala na Utumishi.



*Jarida la* Bunge | Toleo la Kumi na Tatu Septemba 2026



Katika kipindi hicho, Katibu wa Bunge alikuwa Ndg. Elias Kazimoto, ambaye alikuwa Katibu wa tano baada ya Uhuru kati ya makatibu waliolihudumia Bunge hadi sasa.

### Ukuaji wa idadi ya watumishi

Moja ya vipimo muhimu vya ukuaji wa Sekretariat ya Bunge ni ongezeko la idadi ya watumishi. Mwaka 1926, wakati Baraza la Kutunga Sheria lilipoanza, kulikuwa na mtumishi mmoja tu, Katibu wa Baraza. Kufikia mwaka 1953, watumishi walikuwa wawili: Spika wa Baraza na Katibu wa Baraza. Mwaka 1961, watumishi walikuwa 13; Spika, Katibu, makatibu wasaidizi watatu na watumishi wa kada nyingine ambao walikuwa 8

Katika miongo iliyofuata, majukumu ya Bunge yaliongezeka na hivyo mahitaji ya watumishi yakapanuka. Mwaka 1991, watumishi wa Bunge walikuwa 62. Ongezeko hili linaonesha hatua ya kutoka sekretariat ndogo iliyokuwa ikitegemea watendaji wa Serikali kwenda katika muundo wenye kada na huduma nyingi zaidi.

Baada ya kuimarishwa kwa uhuru wa kiutawala na kuanzishwa kwa Tume ya Huduma za Bunge, mahitaji ya watumishi wenye taaluma maalumu yaliendelea kuongezeka. Hivi sasa, mwaka 2026, Bunge lina watumishi 330. Kwa hiyo, ndani ya miaka 100, idadi imeongezeka kutoka mtumishi mmoja hadi 330.

Ukuaji huo haupaswi kutazamwa kama ongezeko la idadi pekee. Bali unaakisi pia upanuzi wa majukumu ya Bunge na kuongezeka kwa huduma zinazohitajika, zikiwemo huduma za kamati, utafiti, maktaba, sheria, bajeti, taarifa rasmi, TEHAMA, mawasiliano, utawala, fedha, usalama, elimu ya uraia na huduma kwa Wabunge.

### Mabadiliko ya Katiba ya mwaka 1992 na

## mfumo wa vyama vingi

Mabadiliko ya Nane ya Katiba ya mwaka 1992 yalirejesha mfumo wa vyama vingi vya siasa. Mabadiliko haya yalikuwa na athari katika utendaji wa Bunge na Ofisi yake. Ofisi ya Bunge ilikoma kuwa sehemu ya usimamizi wa shughuli za uchaguzi; Spika akakoma kuwa Mwenyekiti wa Tume ya Uchaguzi na Katibu wa Bunge akakoma kuwa Mkurugenzi wa Uchaguzi.

Kuanzishwa kwa Tume ya Uchaguzi yenye uongozi wake kulitoa nafasi kwa Ofisi ya Bunge kuelekeza nguvu zaidi katika majukumu yake ya msingi ya kuhudumia Bunge. Wakati huo huo, mfumo wa vyama vingi uliifanya Bunge kuwa na mahitaji mapya ya kiutawala na kitaalamu, hasa katika kuwahudumia Wabunge kutoka vyama mbalimbali.

Katika mazingira haya, ilihitajika Sekretarieti yenye uwezo wa kutoa huduma kwa usawa, weledi na bila kujihusisha na siasa za vyama. Hali hii ilichochea mijadala na hatua zilizofuata kuhusu Bunge kuwa taasisi inayojitegemea.

## Semina Chechemuzi na Kamati ya Haki na Huduma za Bunge, 1996

Semina Chechemuzi kwa Wabunge wa chama tawala na vyama vya upinzani ilifanyika Dodoma tarehe 23 hadi 26 Januari 1996 na ilihusu utendaji wa Bunge chini ya mfumo mpya wa vyama vingi vya siasa. Wakati wa semina hiyo, Wabunge walipata fursa ya kujadili changamoto mbalimbali za huduma na maslahi yao.

Baada ya majadiliano hayo, iliundwa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Haki na Huduma za Bunge. Kamati hiyo ilipewa, pamoja na majukumu mengine, jukumu la kushughulikia suala la Bunge kuwa taasisi inayojitegemea na kuangalia uwezekano wa kuwa na chombo cha kusimamia ajira na maslahi ya Bunge.

Kamati iliwasilisha taarifa yake Bungeni katika kikao cha tatu mwezi Aprili 1996. Taarifa hiyo ikawa sehemu ya msingi wa hatua zilizofuata za kuanzisha mfumo wa huduma za Bunge unaojitegemea zaidi.

## Kuanzishwa kwa Tume ya Huduma za Bunge, 1997

Mwaka 1997 Serikali iliwasilisha Muswada wa Sheria wa Kuanzisha Tume ya Huduma za Bunge. Madhumuni ya muswada yalikuwa kuanzisha chombo cha kusimamia utendaji wa Bunge, hususan ajira, nidhamu na masuala ya utumishi. Pia ulilenga kuhakikisha kuwa Bunge linapata watumishi wenye taaluma na uzoefu unaofaa kwa shughuli zake.

Muswada ulilenga kuondokana na utaratibu ambao watumishi wa Bunge walikuwa watumishi wa Serikali na waliweza kuhamishwa wakati wowote kwenda idara nyingine za Serikali. Mfumo mpya ungewezesha Bunge kujenga utamaduni wa kudumu wa kitaasisi na kuwa na watumishi wanaolenga mahitaji maalumu ya Bunge.

Bunge lilipitisha muswada huo na ukapata kibali cha Rais kuwa Sheria ya Huduma za Bunge, 1997, iliyoanza kutumika tarehe 1 Julai 1997. Kwa mujibu wa sheria hiyo, Tume ya Huduma za Bunge ilipewa jukumu la kuandaa muundo wa uendeshaji bora wa Ofisi ya Bunge.

Kuanzishwa kwa Tume kulikuwa hatua kubwa katika kuimarisha uhuru wa Bunge. Tume iliwezesha Bunge kuwa na udhibiti mkubwa zaidi wa masuala yake ya ndani, yakiwemo rasilimali watu, bajeti na mipango ya kitaasisi.

## Muundo wa kwanza chini ya Tume ya

**Mwaka 1998, Tume iliwasilisha hoja ya muundo mpya wa Ofisi ya Bunge.** Muundo huo ulizingatia mabadiliko yaliyotokana na mfumo wa vyama vingi na mahitaji mapya ya Bunge. Bunge liliidhinisha muundo huo tarehe 24 Aprili 1998.

## Huduma za Bunge

Baada ya kuanzishwa kwa Tume mwaka 1997, muundo mpya wa Ofisi ya Bunge uliandaliwa. Kwa mara ya kwanza kukawa na Idara nne: Idara ya Kamati za Bunge; Idara ya Shughuli za Bunge; Idara ya Maktaba; na Idara ya Utawala na Utumishi.

Idara hizi ziliundwa kwa kuzingatia mahitaji ya kazi. Idara ya Kamati za Bunge ilihudumia kamati mbalimbali, wakati Idara ya Shughuli za Bunge ilihusika na uendeshaji wa shughuli za Bunge, taarifa rasmi, habari na usalama. Idara ya Maktaba ilihudumia maktaba na utafiti, huku Idara ya Utawala na Utumishi ikishughulikia utawala, watumishi, mipango, mafunzo na huduma kwa Wabunge.

Mwaka 1998, watumishi waliokuwa wameazimwa kutoka Serikalini walipewa fursa ya kuamua kama wabaki katika utumishi wa Bunge au warejee Serikalini. Waliobaki wakawa sehemu ya msingi wa wafanyakazi wa kudumu wa Bunge. Hatua hii ilisaidia kujenga kumbukumbu, uzoefu na utamaduni wa kitaasisi.



## Muundo mpya wa Ofisi ya Bunge, 1998

Mwaka 1998, Tume iliwasilisha hoja ya muundo mpya wa Ofisi ya Bunge. Muundo huo ulizingatia mabadiliko yaliyotokana na mfumo wa vyama vingi na mahitaji mapya ya Bunge. Bunge liliidhinisha muundo huo tarehe 24 Aprili 1998.

Muundo huo ulikuwa na Idara tano: Idara ya Maktaba na Utafiti; Idara ya Kamati za Bunge; Idara ya Shughuli za Bunge; Idara ya Taarifa Rasmi; na Idara ya Utawala na utumishi. Kila idara ilipata sehemu kulingana na majukumu yake.

Vitengo pia viliongezeka kutoka viwili hadi vinne, vikiwemo Kitengo cha Habari na Elimu kwa Umma, Kitengo cha Ulinzi na Usalama, Kitengo cha Uhasibu na Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani. Muundo huu uliweka msingi wa kupanua zaidi huduma za kitaalamu katika miaka iliyofuata.

## Muundo wa mwaka 2018

Mwaka 2018 kulifanyika marekebisho ya muundo wa Ofisi ya Bunge yaliyothibitishwa tarehe 7 Julai 2018. Idara zilikuwa sita: Utawala na Rasilimali Watu; Maktaba na Utafiti; Shughuli za Bunge; Kamati za Bunge; Bajeti; na Huduma za Sheria.

Vitengo viliongezeka hadi saba, vikiwemo Mawasiliano na Uhusiano wa Kimataifa, Ulinzi na Usalama, TEHAMA, Fedha na Uhasibu, Manunuzi, Ukaguzi wa Ndani na Taarifa Rasmi za Bunge (Hansard). Pia kulikuwa na Ofisi ndogo ya Bunge Zanzibar iliyokuwa na hadhi inayolingana na idara.

Mabadiliko haya yaliimarisha mgawanyo wa majukumu na kuongeza uwezo wa Ofisi ya Bunge kutoa huduma maalumu katika maeneo muhimu ya shughuli za Bunge.

## Muundo wa mwaka 2024

Muundo wa mwaka 2024 uliendelea kwa msingi wa muundo wa 2018 lakini ulifanyiwa maboresho. Kitengo cha Mawasiliano na Uhusiano wa Kimataifa kiligawanywa na kuwa Kitengo cha Mawasiliano na Elimu kwa Umma pamoja na Kitengo cha Uhusiano wa Kimataifa.

Vilevile, viliongezwa Kitengo cha Menejimenti ya Miliki na Kitengo cha Ufuatiliaji na Tathmini. Mabadiliko haya yanaonesha kwamba Sekretariat inaendelea kubadilika kulingana na mahitaji mapya ya taasisi na mazingira ya utendaji.



*Jarida la* Bunge | Toleo la Kumi na Tatu Septemba 2026

## Idadi ya Watumishi Toka 1926 - 2026

**Mwaka 1926**
Idadi ya Wafanyakazi
*Mfanyakazi Mmoja*
**1**

**Mwaka 1991**
Idadi ya Wafanyakazi
*Wafanyakazi Sitini na Mbili*
**62**

**Mwaka 2026**
Idadi ya Wafanyakazi
*Wafanyakazi Mia Tatu Thelathini*
**330**

### Kuimarisha uhuru, uwajibikaji na weledi

Ukuaji wa Ofisi ya Bunge unahusiana kwa karibu na lengo la kuimarisha uhuru wa Bunge. Bunge lenye ufanisi linahitaji mfumo wa kiutawala unaoweza kutoa huduma za kitaalamu bila kutegemea taasisi nyingine katika masuala ambayo yanapaswa kusimamiwa ndani ya Bunge.

Kwa miaka mingi, mageuzi ya kimiundo yameimarisha uwezo wa Bunge kusimamia mambo yake ya ndani. Kuanzishwa kwa Sekretariat inayowajibika moja kwa moja kwa Bunge kumeongeza mwendelezo wa kitaasisi, uwajibikaji na ufanisi.

Ukuaji wa idadi ya watumishi kutoka mmoja mwaka 1926 hadi 330 mwaka 2026 unaonesha pia ongezeko la utaalamu unaohitajika. Leo Bunge linahitaji wanasheria, watafiti, maktaba, wachumi, wataalamu wa bajeti, TEHAMA, mawasiliano, utawala, fedha, usalama na kada nyingine ili kukidhi mahitaji ya Bunge la kisasa.

### Hitimisho

Ukuaji wa Sekretariat ya Bunge la Tanzania ni sehemu muhimu ya historia ya maendeleo ya Bunge. Safari hii ilianza mwaka 1926 wakati Baraza la Kutunga Sheria lilipokuwa na mtumishi mmoja tu, Katibu wa Bunge. Mwaka 1953 watumishi walikuwa wawili, yaani Spika wa Baraza na Katibu wa Bunge. Kufikia mwaka 1991, idadi ilifika 62, na mwaka 2026 imefikia watumishi 330.

Ongezeko hili la watumishi limeambatana na mabadiliko makubwa ya muundo na hadhi ya Bunge. Kutambuliwa kwa Katibu na Sekretariat kikatiba mwaka 1984, mabadiliko ya mwaka 1992 yaliyotokana na mfumo wa vyama vingi, kuanzishwa kwa Tume ya Huduma za Bunge mwaka 1997, na kuhamia katika mfumo wa ajira ya Bunge mwaka 1998 ni hatua muhimu katika safari ya kujenga taasisi yenye uwezo wa kujitegemea.


Vilevile, maboresho ya miundo ya 2015, 2018 na 2024 yanaonesha kuwa Sekretariat haijabaki katika muundo mmoja, bali imeendelea kubadilika kulingana na mahitaji ya wakati. Ukuaji huu umeongeza uwezo wa Bunge kupata huduma za kitaalamu na kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi.

Kwa ujumla, historia ya Sekretariat inaonesha mabadiliko kutoka ofisi ndogo iliyokuwa na mtumishi mmoja hadi taasisi kubwa yenye watumishi 330 na huduma nyingi za kitaalamu. Ukuaji huu ni msingi muhimu wa Bunge la kisasa na utaendelea kuwa na umuhimu katika kukuza demokrasia, uwajibikaji, uwakilishi na maendeleo ya taifa.





# Hoja Kuhusu Utaratibu Bungeni: Ulinzi Wa Mjadala, Si Kumkatiza Mbunge



*Na. Athuman Hussein, ndc*

a.brambati@bunge.go.tz

*"Desturi na taratibu za Bunge hazipo katika ombwe. Kwa hakika ndizo nguzo kuu za ufanisi wa shughuli za kila siku katika kazi ya Mbunge." -* **John Bercow**

**Hayo ni maneno ya Mheshimiwa John Bercow, aliyewahi kuwa Spika wa Bunge la Wawakilishi (House of Commons) la Uingereza ambayo yanaweka msingi wa makala hii. Jambo muhimu la kuanza nalo ni kuwa, utaratibu wa kibunge si mkusanyiko wa kanuni za kibunge pekee, bali ni mfumo unaowezesha Bunge kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi, haki na utulivu.**

**Sambamba na hilo, ieleweke kwamba, kadiri shughuli za Bunge zinavyokuwa changamano na mazingira ya uendeshaji wake yanavyobadilika, ndivyo umuhimu wa kuelewa na kuzingatia kanuni, desturi na taratibu za kibunge unavyoongezeka. Hayo ndiyo yanayoweka mipaka na kulinda haki ya Mbunge kushiriki katika mjadala bila kuathiri haki za Wabunge wengine wala mwenendo wa Bunge.**

**Katika muktadha huo, hoja "Kuhusu Utaratibu" (Point of Order) ni mojawapo ya nyenzo muhimu za kulinda uadilifu wa kiutaratibu wa shughuli za Bunge. Ingawa inaweza kuonekana kama njia ya kumkatiza Mbunge anayezungumza, dhima yake si kukatiza mjadala wala kupinga maudhui ya hoja, bali kumwezesha Spika au mwongoza kikao mwingine kutambua na inapobidi, kurekebisha ukiukwaji wa Kanuni au utaratibu.**

**Kwa mfano, katika Bunge la Kumi na Moja, Mkutano wa 19, Kikao cha 40, tarehe 8 Juni 2020, Mheshimiwa Mwanne I. Mchemba alisimama kwa hoja "Kuhusu Utaratibu" na kujielekeza kwenye Kanuni ya 64(1) baada ya kauli iliyotolewa kuhusu Wabunge wa Viti Maalum. Kwa maoni yake, kanuni hiyo iliyohusu mambo yasiyoruhusiwa Bungeni, inakiukwa.**

**Naibu Spika aliyekuwa akiongoza kikao, alimsisitiza Mbunge aliyekuwa akichangia azingatie kanuni. Mfano huu unaonesha kwamba hoja "Kuhusu Utaratibu" inaweza kutumika kumkumbusha na kumuomba Mwogoza kikao alishughulikie suala la ukiukaji wa kanuni.**

**Hata hivyo, hoja "Kuhusu Utaratibu" si njia ya Mbunge kuamua mwenyewe kwamba Kanuni imekiukwa. Mbunge huibua suala, Kiongozi wa kikao huchambua na kutoa uamuzi. Hivyo, msingi wa hoja hiyo ni ukiukwaji wa Kanuni au utaratibu. Mbunge anayeibua hoja anatakiwa kuelekeza umakini kwenye jambo mahsusi la kiutaratibu, badala ya**

**Katika kitabu kiitwajo** *Robert's Rules of Order Newly Revised*, utaratibu wa kibunge unaelezwa katika muktadha wa kanuni na misingi inayotawala uendeshaji wa vyombo vinavyofanya uamuzi kupitia majadiliano (*deliberative assemblies*).

kutumia nafasi hiyo kujibu hoja ya Mbunge mwingine, kuingiza hoja mpya au kuendeleza mjadala.

Ili kuelewa hoja "Kuhusu Utaratibu", ni muhimu kwanza kutambua maana ya utaratibu wa kibunge (parliamentary procedure). Kwa ujumla, ni mfumo unaojumuisha kanuni, desturi, vielelezo vya uamuzi uliowahi kutolewa (precedents) na mila za kibunge (conventions) zinzohusu uendeshaji wa Bunge. Kwa hiyo, utaratibu si kufuata hatua kwa mazoea pekee, bali mfumo unaoweka mipaka, majukumu na mamlaka ya washiriki wa shughuli za Bunge.

Katika kitabu kiitwajo *Robert's Rules of Order Newly Revised edition on*, utaratibu wa kibunge unaelezwa katika muktadha wa kanuni na misingi inayotawala uendeshaji wa vyombo vinavyofanya uamuzi kupitia majadiliano (*deliberative assemblies*). Kwa maana hiyo, Bunge linahitaji utaratibu unaowezesha uhuru wa mjadala kuendana na nidhamu na Kanuni zinazotawala mwenendo wa shughuli zake.

Katika muktadha huo, hoja "Kuhusu Utaratibu" ni hoja inayotolewa pale Mbunge anapoona kuwa kuna ukiukwaji wa Kanuni au utaratibu wa Bunge. Madhumuni yake ni kulielekeza suala hilo kwa Spika au kiongozi wa kikao (Kiti) ili litathminiwe na inapobidi, utaratibu urejeshwe. Hivyo, Mbunge anapoibua hoja "Kuhusu Utaratibu", lengo si kupewa nafasi nyingine ya kuchangia, bali kuomba Kiti kichunguze suala mahsusi la kiutaratibu.

Katika hilo, kuna tofauti kati ya hoja "Kuhusu Utaratibu" na kutokubaliana na maudhui ya mjadala inapokuwa muhimu. Mbunge anaweza kutokubaliana kabisa na hoja inayotolewa na Mbunge mwingine. Hata hivyo kutokubaliana huko hakufanyi suala hilo kuwa hoja "Kuhusu Utaratibu".

Kinachofanya hoja kuwa hoja "Kuhusu Utaratibu" ni kuwepo kwa ukiukwaji mahsusi wa Kanuni au utaratibu. Ndiyo maana nafasi ya hoja "Kuhusu Utaratibu" haiwezi kutumiwa kujibu hoja ya Mbunge mwingine, kuingiza hoja mpya au kuendeleza mjadala.

Kwa mujibu wa Erskine May aliyewahi kuwa Katibu wa Bunge la Wawakilishi la Uingereza, hoja "Kuhusu Utaratibu" inahusisha uhusiano wa karibu kati ya jukumu la Kiti la kulinda utaratibu wa Bunge na haki ya Mbunge kuibua ukiukwaji wa utaratibu. Kwa maana hiyo, Hivyo, hoja "Kuhusu Utaratibu" huunganisha haki ya Mbunge kushiriki katika shughuli za Bunge na wajibu wa Kiti kuhakikisha shughuli hizo zinaendeshwa kwa mujibu wa Kanuni.

Katika Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, msingi wa sasa wa hoja "Kuhusu Utaratibu" unatambulika katika Kanuni ya 78 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, 2025. Kanuni hiyo inaweka utaratibu wa Mbunge kuibua hoja "Kuhusu Utaratibu", wajibu wake katika kuibua hoja hiyo na mamlaka ya Spika kuhusu uamuzi.

Kwa utaratibu huo, **Kwanza**, Mbunge anayeibua hoja "Kuhusu Utaratibu" husimama na kutamka maneno "Kuhusu Utaratibu." Hatua hiyo humtaka Mbunge anayezungumza kuketi ili kutoa nafasi kwa Kiti kusikiliza na kushughulikia suala lililoibuliwa. Hii inaonesha kuwa hoja "Kuhusu Utaratibu" ni njia ya kuhitaji Kiti kitambue na kusikiliza hoja mahsusi ya kiutaratibu.

**Pili**, Mbunge anayetoa hoja "Kuhusu Utaratibu" ana wajibu wa kuonesha wazi msingi wa hoja yake, ikiwamo Kanuni au sehemu ya Kanuni inayodaiwa kukiukwa. Hili linaonekana pia katika Bunge la Kumi na Tatu, Kikao cha 21, tarehe 4 Mei 2026, ambapo Mheshimiwa Esther N. Matiko alisimama na kusema "Kuhusu Utaratibu". Kisha akaelekeza hoja yake kwenye Kanuni ya 78. Mfano huu unaonesha kwamba kutamka "Kuhusu Utaratibu" pekee hakutoshi, Mbunge anatakiwa kuonesha msingi wa kiutaratibu kwa hoja yake.

Kwa hiyo, hoja "Kuhusu Utaratibu" haiwezi kutumika kama njia ya kujibu hoja ya Mbunge mwingine, kutoa maoni binafsi, kuanzisha hoja mpya au kuendeleza mjadala. Katika mfano wa Mheshimiwa Esther Matiko, hoja yake ilihusu utaratibu wa matumizi ya lugha katika mchakato wa uchaguzi, badala ya kuingia katika mjadala mpana wa wagombea wenyewe.

Baada ya kueleza hoja yake, Mbunge anatakiwa kuketi na kusubiri uamuzi wa Kiti. Hili linaonekana wazi katika Bunge la Kumi na Mbili, Kikao cha 27 cha tarehe 20 Mei 2022, ambapo Mheshimiwa Benaya Liuka Kapinga alitoa kauli kuhusu "kuondoka na Siwa" wakati wa mjadala. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge na Uratibu, aliibua hoja "Kuhusu Utaratibu" kwa kurejea Kanuni ya 71(j) kuhusu lugha inayotumika ambayo inaweza kukera.



Baada ya Kiti kulishughulikia suala hilo, Mheshimiwa Kapinga alikubali kufuta maneno hayo na kuendelea na mchango wake. Mfano huu unaonesha kwamba hoja "Kuhusu Utaratibu" inaweza kuleta marekebisho ya mwenendo wa mjadala bila kuhitaji kuzuia mjadala mzima.

Kwa upande wa Spika, Kanuni ya 78 inampa mamlaka ya kuamua iwapo suala lililoibuliwa ni hoja "Kuhusu Utaratibu" inayostahili kushughulikiwa. Baada ya kulisikiliza, Spika anaweza kutoa uamuzi papo hapo au, inapobidi, kuahirisha uamuzi ili kupata muda wa kutafakari suala hilo. Hivyo, mamlaka ya Kiti hayaishii kusikiliza tu, bali pia kutathmini uhalali wa hoja ya kiutaratibu na kuamua hatua inayofaa.

Hapa kuna tofauti muhimu kati ya haki ya Mbunge kuibua hoja "Kuhusu Utaratibu" na mamlaka ya Kiti ya kutoa uamuzi juu yake. Mbunge ana haki ya kuielekeza hoja kwa Kiti, lakini si yeye anayeamua kwamba Kanuni imekiukwa. Uamuzi huo ni wa Kiti. Mgawanyo huu ndio unaozuia hoja "Kuhusu Utaratibu" kugeuka kuwa mjadala wa ushindani miongoni mwa Wabunge.

Mamlaka hayo yanaendana na Kanuni ya 5 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, 2025, inayomtaka Spika kuongozwa na Katiba, sheria, Kanuni za Bunge, uamuzi wa awali wa miongoni mwa Maspika pamoja na mila na desturi za Mabunge yanayofuata mfumo wa Westminster. Kwa hiyo, uamuzi wa Kiti haupaswi kutazamwa kama maoni binafsi ya Spika, bali kama matumizi ya vyanzo vinavyotambulika vya utaratibu wa kibunge.

Kwa mtazamo huo, uamuzi wa Spika juu ya hoja "Kuhusu Utaratibu" ni sehemu ya mamlaka ya Kiti ya kusimamia na kutafsiri utaratibu wa Bunge. Hii ndiyo sababu Mbunge anapowasilisha hoja hawezi kulazimisha Kiti kufikia hitimisho analolitaka. Kazi yake ni kuweka suala la kiutaratibu mbele ya Kiti. Kazi ya Kiti ni kulichambua na kutoa mwelekeo.

Kanuni hii inaonekana pia katika mfano wa Bunge la Kumi na Tatu, kikao cha tarehe 4 Mei 2026, ambapo baada ya Mheshimiwa Esther N. Matiko kuibua suala kuhusu utaratibu wa lugha katika uchaguzi, Spika hakufuata moja kwa moja hitimisho lililopendekezwa na Mbunge. Badala yake, Kiti kilielekeza kwenye kanuni inayohusu mamlaka ya Kiti na kusisitiza kwamba uamuzi wa Kiti ni wa mwisho ndani ya Bunge. Mfano huu unaonesha mipaka ya haki ya kuibua hoja "Kuhusu Utaratibu": haki hiyo haimaanishi haki ya kuamuru matokeo ya uamuzi.

Kwa hiyo, kutambuliwa kwa hoja "Kuhusu Utaratibu" katika Kanuni za Kudumu za Bunge la Tanzania kunaonesha kwamba, urithi wa Westminster umeendelezwa ndani ya mfumo wa Tanzania kwa kuweka wazi haki ya Mbunge kuibua suala la kiutaratibu na mamlaka ya Kiti kuliamua. Hivyo, hoja "Kuhusu Utaratibu" hujenga daraja kati ya haki ya Mbunge kushiriki katika mjadala na wajibu wa Kiti kulinda uadilifu wa utaratibu wa Bunge.

Kamwe, hoja "Kuhusu Utaratibu" si kikwazo cha

Mbunge anayeibua hoja

**"Kuhusu Utaratibu" anapaswa kujiuliza:** "Ni Kanuni au utaratibu gani hasa unaodaiwa kukiukwa?" Jibu la swali hilo ndilo linalotenganisha Hoja kuhusu Utaratibu na kutokubaliana na maudhui ya mjadala.

mjadala, bali kinga ya kiutaratibu inayolinda mjadala wenyewe. Inawezesha ukiukwaji wa Kanuni kutambuliwa na kushughulikiwa wakati shughuli za Bunge zikiendelea. Inasaidia kuhakikisha kwamba mjadala unaendelea ndani ya mfumo unaotambuliwa na Bunge.

Jambo la msingi ni kutofautisha mjadala wa maudhui na suala la utaratibu. Mbunge anaweza kutokubaliana kabisa na hoja inayotolewa na Mbunge mwingine, lakini kutokubaliana huko hakufanyi suala hilo kuwa hoja "Kuhusu Utaratibu". Kinachofanya suala kuwa hoja "Kuhusu Utaratibu" ni kuwepo kwa suala mahsusi linalohusu ukiukwaji wa Kanuni au utaratibu.

Kwa mfano, katika Bunge la Kumi na Mbili ya tarehe 20 Mei 2022, hoja ya Mheshimiwa Benaya L. Kapinga ilikuwa imejikita katika utekelezaji wa mradi na fedha zitakavyorejeshwa. Kauli yake kuhusu "kuondoka na Siwa" ndiyo iliyosababisha suala la utaratibu kuibuliwa. Hapa tunaona tofauti kati ya hoja ya msingi ya Mbunge na jambo la kiutaratibu lililohitaji kushughulikiwa na Kiti. Hoja "Kuhusu Utaratibu" haikuingia katika uhalali wa hoja yake kuhusu mradi; ilihusu namna jambo lilivyowasilishwa.

Kwa hiyo, matumizi sahihi ya hoja "Kuhusu Utaratibu" yanahitaji uelewa wa Kanuni, nidhamu ya kibunge na uaminifu katika kuitumia. Inapotumika kwa madhumuni ya kuchelewesha shughuli, kumkatiza mzungumzaji bila msingi wa kiutaratibu au kuingiza hoja mpya, inapoteza dhima yake ya msingi.

Kinyume chake, inapotumika kwa usahihi, hoja "Kuhusu Utaratibu" humsaidia Mbunge kutekeleza haki yake ya kushiriki katika kulinda utaratibu wa Bunge, huku ikikipa Kiti fursa ya kutekeleza wajibu wake wa kusimamia mwenendo wa kikao. Msingi wa ushirikiano huo unatokana na mgawanyo wa majukumu kati ya Mbunge na Kiti.

Uhusiano kati yao katika hoja "Kuhusu Utaratibu" si wa ushindani. Mbunge huibua suala na Kiti hutoa uamuzi. Mgawanyo huu wa majukumu ndio unaofanya utaratibu huo uwe nyenzo ya kulinda nidhamu ya mjadala bila kuathiri mamlaka ya Spika.

Kugawanya majukumu kwa namna hiyo, kuna umuhimu mpana zaidi katika kulinda uadilifu wa mchakato wa Bunge (*procedural integrity*). Hoja "Kuhusu Utaratibu" inahakikisha kwamba, shughuli za Bunge haziendeshwi kwa utashi wa mtu binafsi, bali ndani ya mfumo wa Kanuni na taratibu unaotumika kwa wote.

Uadilifu huo wa mchakato ndio unaoifanya nidhamu ya utaratibu kuwa sehemu ya uhalali wa mjadala wa Bunge. Uhalali huo hautokani na uhuru wa kuzungumza pekee, bali na uhuru huo kutekelezwa ndani ya utaratibu unaolinda haki za Wabunge wote, mamlaka ya Kiti na heshima ya Bunge.

Kwa hiyo, Mbunge anayeibua hoja "Kuhusu Utaratibu" anapaswa kujiuliza: "Ni Kanuni au utaratibu gani hasa unaodaiwa kukiukwa?" Jibu la swali hilo ndilo linalotenganisha hoja "Kuhusu Utaratibu" na kutokubaliana na maudhui ya mjadala.

Kwa upande wa Kiti, jukumu ni kuchambua hoja hiyo kwa kuzingatia Kanuni, uamuzi wa awali wa Maspika waliotangulia na misingi ya utaratibu wa kibunge, kisha kutoa mwelekeo unaofaa. Hapo ndipo haki ya Mbunge kuibua suala inapokutana na mamlaka ya Kiti ya kulinda utaratibu wa Bunge.

Kwa mtazamo huo, hoja "Kuhusu Utaratibu" ni kinga ya mjadala, si kikwazo chake. Inapotumika kwa usahihi, humwezesha Mbunge kushiriki kwa uhuru ndani ya mipaka ya Kanuni, huku Kiti kikilinda utaratibu na usawa wa mjadala.

Hatimaye, thamani ya hoja "Kuhusu Utaratibu" haipimwi kwa uwezo wake wa kukatiza mjadala, bali kwa mchango wake katika kulinda uadilifu wa mchakato wa Bunge. Inapotumika ndani ya mipaka ya Kanuni, hulinda haki ya Mbunge kuzungumza, huimarisha mamlaka ya Kiti na kuhakikisha uhuru wa mjadala unaenda sambamba na nidhamu ya kiutaratibu.

Penye utaratibu, ndipo haki ya kusikilizwa na haki ya kuamua hupata uhalali. Hoja "Kuhusu Utaratibu" si kumkatiza Mbunge, ni kulinda mjadala ambao kila Mbunge ana haki ya kushiriki.







# Ndoto ya Sheria Ndogo:

## *Safari ya Kutafuta Dhamira ya Bunge katika Mamlaka Yaliyokasimiwa*

**Na.** Athumna Hussein *ndc*

a.brambati@bunge.go.tz

**Sheria ndogo mara nyingi huonekana kama mkusanyiko wa vifungu vya kanuni za wizara, kanuni za uendeshaji, kanuni za taasisi au sheria ndogo za Halmashauri, ambavyo vimeandikwa kwa ufundi wa uandishi wa sheria. Lakini nyuma ya kila kifungu au kanuni kuna mamlaka yaliyotolewa na Bunge, mipaka iliyowekwa na sheria mama na hatimaye, athari kwa mwananchi. Kwa sababu hiyo, uchambuzi wake si zoezi la kutafuta makosa pekee, ni sehemu ya kuhakikisha kuwa mamlaka yaliyokasimiwa yanatumika kwa madhumuni na ndani ya mipaka iliyokusudiwa.**

Usiku mmoja, baada ya siku ndefu ya kupitia Rasimu ya Taarifa ya Kamati ya Bunge ya Sheria Ndogo na nyaraka za kisheria iliyowasilishwa kwangu na Sekretarieti, nilikaa mezani nikiwa nimezungukwa na majalada kadhaa. Baadhi yalikuwa na nakala za sheria ndogo, mengine yakiwa na vifungu vya sheria mama vilivyoweka mamlaka ya kutunga sheria hizo na mengine yakiwa na maswali ya kisheria niliyokuwa nikijaribu kuyapatia majibu.

Nilifungua jalada moja nikapitia kifungu baada ya kifungu kisha nikahamia jalada lingine. Kila nilipojaribu kufunga jalada moja, swali lingine lilijitokeza kutoka kwenye jalda lingine. Hatimaye, nikayaacha majalada kadhaa yakiwa wazi juu ya meza, huku baadhi ya vifungu vikiwa vimewekewa alama kwa kalamu.

Lakini jambo moja halikuacha kunisumbua. Kwa nini Bunge linapaswa kujihushisha na sheria ndogo zilizotungwa na mamlaka mbalimbali serikalini? Niliwaza swali hilo kwa muda. Baadye, uchovu ukanishinda. Niliinuka na kuelekea kitandani, nikiziacha zile nyaraka zikiwa wazi juu ya meza.

Mara tu usingizi uliponichukua, nilijikuta katika ukumbi mkubwa wa ajabu nikiwa nimesimama mbele ya lango kubwa ambalo sikuwahi kuliona katika maisha yangu. Juu yake kulikuwa na maandishi: "Mamlaka ya Bunge". Nilitazama kulia na kushoto. Hakukuwa na mtu. Kulikuwa na ukimya mzito, ule ukimya unaomfanya mtu asikie hata sauti ya mawazo yake mwenyewe.

Nilipojaribu kulisogelea lango, sauti ikasikika nyuma yangu. "Unajua mamlaka iliyokufikisha hapa?" Niligeuka. Mbele yangu alisimama mzee mwenye uso wa utulivu na macho yaliyobeba siri nyingi. Mkono wake wa kuume ulikuwa umeshika kitabu kikubwa kilichoandikwa "Katiba".

> **Tulipofika mbele ya lango lingine, alisimama. Juu yake kulikuwa na maandishi makubwa:** MAMLAKA YALIYOKASIMIWA. Mlinzi akanyanyua mkono wake wa kuume na kuligusa lango. Mara, maandishi yale yakaanza kung'aa. **"Unajua kwa nini mahala hapa ni muhimu?" aliuliza.**

"Ni mamlaka ya Bunge," nilijibu kwa kusita. Akatabasamu. "Basi leo utajifunza jambo moja muhimu: Bunge linapokasimu mamlaka, halikabidhi dhamira yake." Lango likafunguka taratibu.

Na hapo safari yangu ya sheria ndogo ilianza. Sikuwa najua kwamba nyuma ya lango lile kulikuwa na safari ya kufuatilia mamlaka: ilipotoka, ilivyotumika, mipaka yake na hatimaye namna ilivyomfikia mwananchi.

Nilimfuata Mlinzi wa Utawala wa Sheria bila kujua kwamba kila hatua tunayopiga ingeibua swali lipya. Nikauliza, Je, sheria ndogo ni utekelezaji wa sheria mama au ni mamlaka iliyovuka mipaka yake? Kisha nikamtazama Mlinzi kwa muda, lakini hakujibu mara moja. Aligeuka na kuanza kutembea akielekea upande wa pili wa ukumbi. Nikamfuata.

Tulipofika mbele ya lango lingine, alisimama. Juu yake kulikuwa na maandishi makubwa: MAMLAKA YALIYOKASIMIWA. Mlinzi akanyanyua mkono wake wa kuume na kuligusa lango. Mara, maandishi yale yakaanza kung'aa. "Unajua kwa nini mahala hapa ni muhimu?" aliuliza.

"Kwa sababu Bunge haliwezi kutunga kila kanuni na kila sharti linalohitajika katika utekelezaji wa sheria?" nilijibu. "Ndiyo," alikubali. "Lakini hiyo ni nusu tu ya jibu." Alinitazama kwa makini na kusisitiza.

"Bunge linapokasimu madaraka kwa Waziri au chombo kingine, halifanyi hivyo kwa kumaanisha linampa uhuru wa kufanya chochote anachotaka. Linampa mamlaka kwa madhumuni fulani, ndani ya mipaka fulani na kwa masharti fulani." Lango likafunguka kwa kishindo chepesi.

Ndani yake kulikuwa na ukumbi mpana. Katikati yake kulikuwa na mzani mkubwa. Upande mmoja uliandikwa: MAMLAKA na upande mwingine: MIPAKA. Nilisogea karibu. "Lakini kama mamlaka tayari yametolewa, kwa nini yapimwe tena?" niliuliza.

Mlinzi akatabasamu. "Kwa sababu," alisema kwa sauti ya taratibu, "mamlaka yaliyokasimiwa hayakabidhiwi bila kikomo. Mipaka huenda nayo." Maneno yale yalining'inia hewani kwa muda.

Kisha akanionesha kitabu alichokuwa ameshika. "Sheria mama ndiyo huweka chanzo cha mamlaka, humtaja anayekabidhiwa, huainisha anachoruhusiwa kufanya na huweka mipaka ya mamlaka hayo."

Akaweka kitabu juu ya mzani. Ghafla, upande ulioandikwa MAMLAKA ukashuka na ulioandikwa MIPAKA ukapaa. Nilishangaa. "Unaona?" alisema. "Hata mamlaka iliyopewa na sheria ina uzito wake. Lakini uzito huo hauwezi kuzidi mipaka iliyowekwa na sheria mama." Akachukua jalada moja kutoka mezani na kunikabidhi. "Usiangalie tu kinachosemwa na sheria hii. Tafuta kwanza kile kilichoruhusiwa kusemwa."

Nilifungua jalada."Anza hapa," alisema. Mamlaka haya yametoka wapi? Nilitazama kifungu cha kwanza. Kisha cha pili. Kisha cha tatu. Kila kifungu kilionekana kunipeleka nyuma zaidi: kutoka kwenye sheria ndogo kwenda kwenye sheria mama na kutoka kwenye sheria mama kwenda kwenye mamlaka yaliyokasimiwa.

"Na ukishajua yametoka wapi?" niliuliza. Mlinzi akatabasamu. "Uliza swali la pili." Akanielekeza, nikauliza. "Yametumika kwa madhumuni yaliyokusudiwa?" Mlinzi hakujibu. Nilitazama lango lililokuwa mbele yetu. Juu yake sasa kulikuwa na maneno mapya: Mamlaka yaliyokasimiwa si Uhuru usio na Mipaka.

Mlinzi akalisukuma. "Twende," alisema. "Huko ndiko tunakoanza kuona tofauti kati ya kutekeleza sheria na kuandika sheria nyingine kwa jina la sheria ndogo." Lango likafunguka.

Nyuma yake kulikuwa na ukumbi mwingine mrefu, wenye milango mingi. Kila mlango ulikuwa na swali lake. Je, mamlaka yametumika ndani ya mipaka? Je, madhumuni yake yameheshimiwa? Je, haki za mwananchi zimezingatiwa? Je, sharti hili lina msingi wa sheria? Nilimtazama Mlinzi.

"Kwa nini maswali ni mengi hivi?" Akasimama na kunitazama. "Kwa sababu," alisema, "sheria ndogo inaweza kuwa na maneno machache, lakini mamlaka inayobeba inaweza kubadilisha maisha ya wengi." Kisha akaendelea mbele. Mimi nikamfuata. Safari ilikuwa bado ndefu.

Mbele yetu kulikuwa na lango lingine. Juu yake kuliandikwa: Mipaka ya Mamlaka. Mlinzi akalisogelea na kulifungua taratibu. "Hatua ya kwanza," alisema, "ni kujua mamlaka yametoka wapi". Hatua ya pili ni kuangalia kama yametumika ndani ya mipaka iliyowekwa."

Nilitazama ndani ya lango lile. "Na tukikuta yamevuka mipaka?" Mlinzi akageuka na kunitazama. "Basi hapo ndipo tunapoanza kuuliza kama sheria ndogo hii imetekeleza sheria mama au imejipa mamlaka ambayo haikukabidhiwa au kukasimiwa."Tukaingia.

Safari ya uchambuzi ilikuwa imeanza kweli. Lakini Mlinzi hakuniruhusu niende moja kwa moja kwenye orodha ndefu ya vigezo. Badala yake, alisimama mbele ya lango lingine na kunitazama kwa utulivu.



Jarida la Bunge | Toleo la Kumi na Tatu Septemba 2026

"Ni rahisi kusema mamlaka imevuka mipaka," alisema. "Lakini je, unaweza kuitambua mipaka hiyo inapovukwa?" Kisha akanionesha tukio moja lililokuwa mbele yetu.

Ndipo nilipoanza kuelewa kwamba, uchambuzi wa mamlaka hauishii katika kuuliza kama mamlaka yametolewa. Lazima pia kujiuliza: yametumika ndani ya mipaka gani, kwa madhumuni gani na kwa kiwango gani?

Tulipovuka lango lile, niliona tena mzani katikati ya ukumbi. Upande mmoja uliandikwa sheria mama, mwingine sheria ndogo. Mlinzi akasimama.

"Angalia kwa makini," alisema. Akaweka kitabu cha Katiba upande wa kwanza wa mzani, kisha sheria mama katikati na jalada la sheria ndogo upande wa pili. "Katiba ndiyo msingi wa juu. Sheria mama ndiyo inayotoa mamlaka. Na sheria ndogo lazima ibaki ndani ya mipaka ya mamlaka hayo." Akainama kidogo na kuutazama mzani.

"Ikiwa sheria ndogo inakwenda zaidi ya mamlaka iliyotolewa na sheria mama, tunaanza kujiuliza: Je, mamlaka yamevuka mipaka?"

Nilimtazama bila kusema. "Na hapo tunakutana na neno moja muhimu," akaendelea. Akaandika kwenye hewa: "Ultra Vires." Yaani, kufanya jambo au hatua nje ya mamlaka yaliyotolewa.

Mlinzi akafungua kitabu kingine. "Hiki," alisema, "ni Sheria ya Tafsiri ya Sheria, Sura ya 1". Hapa tunajifunza namna sheria zinavyosomwa, kufasiriwa na kutekelezwa. Vifungu vyake vya tafsiri hutupatia msingi wa kuelewa maana ya maneno na masharti ya sheria; lakini tunapofika kwenye sheria ndogo, kitabu hiki kinazungumza kwa sauti iliyo wazi zaidi.

Akageuza kurasa. "Kifungu cha 36 kinatukumbusha kwamba sheria ndogo haiwezi kwenda kinyume na sheria iliyoipa mamlaka. Kifungu cha 39 kinatuelekeza kwamba maneno yaliyotumika katika sheria ndogo yasomwe kwa maana yake katika sheria mama.

"Na pale mamlaka ya kutunga sheria ndogo yanapotolewa, vifungu vinavyohusu uwasilishaji, uchapishaji na utekelezaji wake hutusaidia kuona kama sheria hiyo imetembea katika njia iliyowekwa na sheria mama." Aliongeza.

Akatulia, kisha akafungua ukurasa mwingine. "Lakini usiangalie vifungu hivi kama orodha ya masharti tu. Vione kama alama za mipaka." Akagusa ukurasa wa 36 kwa kidole. "Hapa tunajiuliza: Je, sheria ndogo imebaki ndani ya sheria mama?"

Akagusa ukurasa wa 39. "Hapa: Je, maneno yake yanaendelea kubeba maana iliyokusudiwa na sheria iliyoiwezesha?" Kisha akagusa ukurasa unaohusu athari za kufutwa kwa sheria mama. "Na hapa, chanzo cha mamlaka kikiondoka, nini kinatokea kwa sheria ndogo iliyotokana nacho?" Akafunga kitabu taratibu.

"Hapo sasa unaona ukweli kuwa Sheria ya Tafsiri ya Sheria si kamusi ya maneno ya kisheria tu. Ni sehemu ya ramani inayotusaidia kufuatilia chanzo cha mamlaka, maana yake, mipaka yake na hatima ya sheria ndogo inayotokana nayo." Alisema.

Mlinzi akaendelea mbele. Mimi nikamfuata, sasa nikiwa na swali jipya kichwani: Je, sheria hii inatekeleza mamlaka yaliyotolewa, au inatumia mamlaka hayo kuunda jambo lipya? Mlinzi akasimama.

"Na hapa," alisema, "ndipo tunapokumbuka kwamba safari hii si ya kisheria tu. Ni ya kibunge."Akaonesha kitabu chake cha Katiba, kisha akafungua ukurasa mwingine.

"Fasili ya 10 ya Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Bunge," alisema, "kimeipa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo jukumu la kuchunguza sheria ndogo na kujiridhisha kwamba inaendana na Katiba, sheria mama na sheria nyingine za nchi." Akatulia kidogo.

"Kwa hiyo, kila tunapoweka sheria ndogo juu ya mizani hii, hatuulizi tu kama imetungwa. Tunauliza pia kama imebaki ndani ya mipaka ya mamlaka iliyotolewa."

"Hivyo, kila tunapouliza kama mamlaka yamevuka mipaka, hatuulizi kwa udadisi. Tunauliza kwa kutimiza jukumu ambalo Bunge lenyewe limeweka." Nilitazama mbele. Kwenye ukuta kulikuwa na maandishi: MAMLAKA - MIPAKA -HAKI - ATHARI**.**

"Lakini mamlaka si kipimo pekee," alisema. "Tunapaswa kuangalia pia madhumuni ya mamlaka, haki za mwananchi, uhakika wa sheria, adhabu, ada na tozo, uwezekano wa utekelezaji na athari kwa maslahi ya umma." Niliona milango ile ikifunguka mmoja baada ya mwingine.

"Kwa hiyo," niliuliza, "haya ndiyo maswali ambayo Kamati inapaswa kujiuliza?" "Ndiyo," akasema. "Lakini si maswali ya kujaza jedwali tu. Ni lenzi za Bunge za kuona kama mamlaka yaliyokasimiwa bado yanatumika kwa uaminifu."

Kisha akafunga kitabu. "Na sasa," alisema, "tumeufikia mwisho wa safari." Nilitazama nyuma. Milango yote tuliyopita ilikuwa bado wazi. Ndipo nilipotambua kwamba kila mlango ulikuwa umeuliza swali lilelile kwa sura tofauti: "Je, mamlaka yaliyokasimiwa bado yanatumika kwa dhamira na

mipaka iliyowekwa na Bunge?" Ukumbi ukatulia.

Safari ya sheria ndogo haikuwa safari ya kutafuta makosa katika vifungu. Ilikuwa safari ya kutafuta dhamira ya Bunge ndani ya mamlaka yaliyokasimiwa.

Mlinzi akafunga kitabu chake. "Na sasa," alisema, "umejua siri ya safari hii."


"Ni ipi?" niliuliza. Akatabasamu. "Mamlaka yanapokasimiwa, wajibu wa kuyasimamia hauondoki." Kabla sijajibu, ukumbi ukaanza kufifia. Milango, mizani na Mlinzi mwenyewe vikaanza kutoweka. Nikafumbua macho.

Nilishtuka kutoka usingizini kwa muda nilibaki kitandani nikitizama 'diary', nikijaribu kutofautisha ndoto na uhalisia. Kisha nikageuka kuelekea mezani. Majalada yaleyale yalikuwa bado yamefunguka.

Lakini safari hii macho yangu yalikwama kwenye kifungu nilichokuwa nimeacha wazi kabla ya kulala. Kwa mara ya kwanza nilikiona kwa namna tofauti.

Kutoka kwenye ndoto hiyo, nilibaki na funzo moja: uchambuzi wa sheria ndogo si kutafuta makosa katika vifungu pekee. Ni kufuatilia chanzo cha mamlaka, madhumuni yake, mipaka yake, haki na athari zake kwa mwananchi. Hapo ndipo jukumu la Kamati linapopata maana yake ya kibunge.

Kwa hiyo, swali la msingi linabaki: mamlaka haya yametoka wapi, yameishia wapi na bado yanaakisi dhamira ya Bunge?







# Hoja za Ukaguzi: Maswali hadi Majibu - Uwajibikaji Bungeni

**Tanbihi ilibainishwa kwamba,**

**'hoja ya ukaguzi' si hukumu ya jinai na wala si uthibitisho wa moja kwa moja." Ilielezwa kuwa "hoja ya ukaguzi" ni suala linalohitaji maelezo, ushahidi na hatua stahiki.**

**Na.** Athumna Hussein *ndc*

a.brambati@bunge.go.tz

*"Ishara ya akili iliyokomaa ni uwezo wa kulichunguza wazo bila kulikubali mara moja"* – **Aristoto.**

Kauli hiyo ya Mwanafalsafa inatutaarifu kwamba, kutambua jambo tunalolijua ni hatua moja na kutambua kile ambacho tunahitaji kukifahamu ni mwanzo wa kutafuta majibu. Imetajwa hivyo kwa sababu katika Toleo lililopita, ufafanuzi kuhusu hoja za ukaguzi ulianza.

Tanbihi ilibainisha kwamba, "hoja ya ukaguzi" si hukumu ya jinai na wala si uthibitisho wa moja kwa moja. Ilielezwa kuwa "hoja ya ukaguzi" ni suala linalohitaji maelezo, ushahidi na hatua stahiki.

Hitimisho katika toleo lililopita liliacha maswali matatu muhimu ambayo ni: Hoja za ukaguzi zina ujumbe gani kwa Bunge? Kwa nini Kamati za Bunge huwaita maafisa masuuli badala ya kuwapeleka moja kwa moja Polisi hadi Magereza? na Mchakato wa kibunge wa kushughulikia hoja za ukaguzi huanzia wapi na kuishia wapi?

Maswali hayo ndiyo yanayoanzisha mwendelezo katika toleo hili. Kwa kuwa hoja za ukaguzi ni mwanzo wa mchakato muhimu katika uwajibikaji, hatua inayofuata si kutoa hukumu, bali kutafuta majibu, kuyapima dhidi ya ushahidi na kuhakikisha kwamba majibu hayo yanazaa hatua za uwajibikaji. Hivyo, Toleo hili linaendeleza safari ya ukaguzi: kutoka kwenye hoja, kwenda kwenye majibu na kutoka kwenye majibu kwenda kwenye hatua.

Neno hatua hapo lina maana ya tendo linalopaswa kutekelezwa ili kuinusuru hali fulani. Kwa msingi huu, kutoka kwenye majibu kwenda kwenye hatua ndiyo kiini hasa cha kazi ya Bunge kusimamia matumizi ya fedha za umma.

Hoja ya ukaguzi kwenye ripoti za ukaguzi zinazowasilishwa Bungeni, hazipaswi kuchukuliwa kama hitimisho la jambo, bali wito wa kutafuta ukweli na majibu.

Hapo ndipo nafasi ya Kamati za Bunge inapopata umuhimu. Kamati huanza kwa kuichambua hoja, kuelewa mazingira yaliyosababisha kuibuka kwake na kisha kuwaita maafisa masuuli na wadau wengine wanaoweza kutoa maelezo au ushahidi unaohitajika.

Hatua hii ya Kamati kuchambua taarifa zilizokaguliwa kwa kuwahoji maafisa masuuli ina msingi wa kikatiba. Ibara ya 63(2) ya Katiba imelipa Bunge madaraka ya kuisimamia na kuishauri Serikali. Katika kutekeleza madaraka hayo, Ibara ya 96 imelipa Bunge uwezo wa kuunda Kamati za namna mabalimbali kwa ajili ya utekelezaji bora wa madaraka yake.

Kamati zinazosimamia matumizi ya fedha za umma na Kamati nyingine za Kudumu za Bunge, zimeundwa kwa mujibu wa Kanuni ya 140 ya Kanuni za Kudumu za Bunge. Katika kutekeleza utekelezaji wa majukumu yake, Kamati zinazosimamia matumizi ya fedha za umma zimepewa msingi wa kazi zake ulioelezwa na Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Bunge.

Kwa kuzingatia msingi huo, Kamati hufanya kazi kwa kuwaita maafisa masuuli. Neno "masuuli" lina maana ya "anayewajibika kwa masuala yote yanayohusu uendeshaji, usimamizi na uidhinishaji wa fedha."

Kwa maana hiyo, Kamati zinapowaita maafisa masuuli zinatafuta maelezo yao kuhusu hatua zilizochukuliwa. Zinafanya hivyo kuliwezesha Bunge kutekeleza sehemu ya jukumu la kuisimamia Serikali kwa kusimamia matumizi ya rasilimali.

Hivyo, kuwaita na kuwahoji maafisa masuuli

Jarida la Bunge | Toleo la Kumi na Tatu Septemba 2026

kusichukuliwe kuwa ishara kwamba wana hatia. Hiyo ni sehemu ya utaratibu wa kibunge wa kutafuta maelezo, kuhakiki ukweli na kutathmini hatua zilizochukuliwa na Serikali.

Kamati hazihitaji kufahamu kilichobainishwa na CAG pekeyake bali pia nini kilitokea, kwa nini kilitokea, nani alikuwa na wajibu wa kuzuia au kurekebisha hali hiyo na ni hatua gani zimechukuliwa baada ya hoja kubainishwa.

Jukumu hilo linaeleweka vizuri kwa muktadha wa Sheria ya Fedha za Umma, Sura ya 348. Kifungu cha 9 cha sheria hiyo kinampa Afisa anayehusika "masuuli" katika chombo, asasi, taasisi au wizara kwa kadiri itakavyokuwa. Hivyo, Kamati inapomwita Afisa "masuuli" haimwiti kwa sababu yeye ndiye aliyethibitika kuwa na kosa, bali yeye ni mhusika mwenye "masuuli" katika chombo au asasi ya kiutawala.

Ikumbukwe kuwa neno "masuuli" hapo lina maana ya "uwajibikaji kwa masuala yote yanayohusu uendeshaji, usimamizi na uidhinishaji wa fedha katika chombo cha kiutawala". Ufafanuzi huo, unatofautisha kati ya mambo mawili: Kuhoji kibunge kuhusu hoja za ukaguzi na hukumu ya kisheria. La kwanza linafanyika kwa madhumuni ya uwajibikaji, lakini la pili linamadhumuni ya adhabu kwa mujibu wa sheria.

Tofauti hizo zinatokana na michakato, misingi na utaratibu ambavyo kwa pamoja vimezingatia mgawanyo wa madaraka miongoni mwa Bunge, Mahakama na mamlaka ya utendaji (Serikali).

Katika muktadha wa uwajibikaji kuna tofauti kati ya hoja ya ukaguzi, jibu la taasisi na uwajibikaji. Hoja huibua swali, jibu hutoa maelezo, ushahidi husaidia kuthibitisha maelezo ya jibu na hatua huonesha kama uwajibikaji umefanyika.

Yote haya yanatujulisha kwamba, kupokea jibu kwenyewe hakutoshelezi hitimisho. Kinachohitajika zaidi baada ya jibu ni ushahidi kama hatua stahiki zimechukuliwa na kama hatua hizo zimeleta mabadiliko yanayoweza kuthibitishwa. Kwa mtazamo huu, safari ya hoja za ukaguzi ni mithili ya mnyororo unaoanzia kwenye hoja, swali, maelezo, ushahidi, uchambuzi, hatua na hatimaye maboresho.

Kila hatua ya mnyororo huo ina umuhimu wake na hakuna inayopaswa kurukwa. Hii ni kwa sababu lengo la mwisho la kuhoji si kupata majibu ya kumaliza mjadala bali kuhakikisha kwamba majibu hayo yanazaa hatua zinazolinda rasilimali za umma na kuimarisha uwajibikaji.

> **Ibara ya 143(5)** inatambua pia majukumu na madaraka mengine ya CAG yatakayoainishwa na sheria. **Kwa msingi huo, Sheria ya Ukaguzi wa Umma, Sura ya 418, inafafanua kwa undani namna mamlaka hayo yanavyotekelezwa.** Kifungu cha 10(1) kinaainisha majukumu ya CAG ya uchunguzi na ukaguzi wa hesabu, huku kifungu cha 34 kikiweka utaratibu wa kuandaa na kuwasilisha ripoti za ukaguzi, ikiwemo kuiwasilisha ripoti ya mwisho ya ukaguzi Mezani mbele ya Bunge.

Kwa maelezo hayo swali muhimu linalofuata si tena "Hoja ya ukaguzi ni nini?" bali „Hoja ya ukaguzi inapofika Bungeni, nini kinachofanyika kwake?".

Kulijibu swali hilo, kunahitajika uelewa kuhusu mambo makuu manne: Mosi: ni nafasi ya Kamati za Bunge inayohusika na Pili: ni mamlaka ya Kamati kuhoji. Mengine mawili: ni wajibu wa Maafisa masuuli kutoa maelezo, na La nne: ni namna Bunge linavyotoka kwenye hoja inayobainishwa hadi hatua ya uwajibikaji.

Yote hayo yanahusu hoja za ukaguzi kama sehemu ya uwajibikaji. Uelewa wa mambo hayo manne unajenga uwezo wa kujibu swali "Hoja ya ukaguzi inapofika Bungeni, Bunge linaifanya nini?".

Kulijibu swali hilo, ifahamike kwamba hoja ya ukaguzi ni zaidi ya orodha ya dosari zilizobainishwa wakati wa ukaguzi. Hoja ya ukaguzi inalitaarifu Bunge kuhusu maeneo ambayo utekelezaji wa shughuli za Serikali, usimamizi wa fedha za umma au mifumo ya udhibiti yanahitaji maelezo, marekebisho au ufuatiliaji zaidi.

Kwa kawaida, hoja za ukaguzi hubainishwa katika Ripoti za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG). Msingi wa ripoti hizo unatokana na Katiba yenyewe.

Ibara ya 143(1) inaweka nafasi ya Mdhibiti na CAG, huku Ibara ya 143(2)(c) ikimtaka, angalau mara moja kila mwaka, kukagua na kutoa taarifa kuhusu hesabu za Serikali ya Jamhuri ya Muungano, hesabu zinazosimamiwa na watumishi wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano, hesabu za Mahakama zote ya Jamhuri ya Muungano na hesabu zinazosimamiwa na Katibu wa Bunge.

Lakini mamlaka ya CAG hayaishii kwenye kuandaa ripoti. Katiba pia inaweka utaratibu wa kuhakikisha ripoti hizo zinafika Bungeni. Kwa mujibu wa Ibara ya 143(4), CAG huwasilisha taarifa kwa Rais, ambaye huwaagiza wahusika kuiwasilisha katika kikao cha kwanza cha Bunge kitakachofanyika baada ya kuipokea, ndani ya muda uliowekwa na Katiba. Hivyo, kuifikisha Ripoti ya CAG Bungeni, ni sehemu ya utaratibu wa kikatiba.

Ibara ya 143(5) inatambua pia majukumu na madaraka mengine ya CAG yatakayoainishwa na sheria. Kwa msingi huo, Sheria ya Ukaguzi wa Umma, Sura ya 418, inafafanua kwa undani namna mamlaka hayo yanavyotekelezwa. Kifungu cha 10(1) kinaainisha majukumu ya CAG ya uchunguzi na ukaguzi wa hesabu, huku kifungu cha 34 kikiweka utaratibu wa kuandaa na kuwasilisha ripoti za ukaguzi, ikiwemo kuiwasilisha ripoti ya mwisho ya ukaguzi Mezani mbele ya Bunge.

Kwa msingi huo, hoja ya ukaguzi haipaswi kutazamwa kama taarifa ya kawaida ya kitaalamu ya CAG. Ni nyenzo inayoliwezesha Bunge kutekeleza jukumu lake la usimamizi na uwajibikaji wa matumizi ya rasilimali za umma. Hoja huibua jambo lililobainika wakati wa ukaguzi, linalohitaji maelezo, uthibitisho, marekebisho au hatua nyingine stahiki za kibunge.

Hata hivyo, hapa kuna tofauti muhimu inayopaswa kueleweka: hoja ya ukaguzi si hukumu wala uthibitisho wa mwisho wa kosa au hatia. Ni jambo lililobainika katika mchakato wa ukaguzi linalohitaji majibu na inapobidi, hatua. Iwapo ukaguzi unabaini viashiria vya udanganyifu, ubadhirifu au kosa lingine lenye athari za kisheria au jinai, suala hilo linaweza kuhitaji uchunguzi na hatua zaidi kwa mujibu wa sheria na mamlaka inayohusika.

Kwa hiyo, jukumu la Bunge si kuchukua nafasi ya vyombo vya uchunguzi au Mahakama, bali kuhakikisha kuwa jambo lililoibuliwa linapata majibu na hatua inayostahili. Ndiyo maana thamani ya hoja ya ukaguzi haipaswi kupimwa kwa kuuliza tu, "Nani amekosea?" Swali la msingi kwa Bunge ni pana zaidi: Nini kimebainika? Kwa nini kimetokea? Nani anawajibika? Hatua gani zimechukuliwa? Na nini kifanyike ili kisijirudie?

Maswali hayo ndiyo yanayoipa hoja ya ukaguzi maana ya kibunge. Inapofika Bungeni, hoja huibua swali; swali huhitaji maelezo; maelezo huhitaji ushahidi; na ushahidi huhitaji uchambuzi. Hapo Kamati inakuwa na nafasi ya kuwaita maafisa masuuli, kuhoji, kuomba nyaraka na kutathmini majibu yaliyotolewa. Pale inapobidi, Kamati inaweza kupendekeza au kusisitiza hatua za kiutawala, kitaasisi au kisheria kwa mujibu wa mamlaka inayohusika.

Kwa maana hiyo, safari ya hoja ya ukaguzi si kutoka kwenye ripoti moja kwa moja kwenda kwenye adhabu. Ni safari inayopita katika hatua za hoja, swali, maelezo, ushahidi, uchambuzi, hatua, utekelezaji na maboresho. Lengo la mwisho si kuongeza idadi ya hoja zilizoshughulikiwa kibunge, bali kuhakikisha kuwa kasoro iliyobainika inasababisha hatua inayofaa na, inapowezekana, marekebisho ya mfumo ili tatizo lisijirudie.

Kwa hiyo, hoja ya ukaguzi si mwisho wa hadithi, ni mwanzo wa safari ya uwajibikaji. Thamani yake ya kweli haipo katika idadi ya hoja zilizotolewa, bali katika majibu yanayopatikana, hatua zinazochukuliwa na maboresho yanayofikiwa. Kama anavyosema mwanafikra mashuhuri Albert Einstein, "The important thing is not to stop questioning." Yaani "jambo la muhimu si kuacha kuhoji'.

Kwa Bunge, swali si mwisho wa mchakato, ni mwanzo wa uwajibikaji. Hoja ikibaki kwenye karatasi, ni kumbukumbu; ikizaa swali, inakuwa uchambuzi; ikizaa hatua, inakuwa uwajibikaji; na ikibadilisha mfumo, inakuwa matokeo. Hapo methali isemayo, "Ukweli unauma, lakini ndio unaotibu", inapata maana yake halisi.

Hoja ya ukaguzi inaweza kuibua jambo lisilopendeza, lakini ikiwa Bunge litaligeuza kuwa swali, swali kuwa ushahidi, ushahidi kuwa hatua na hatua kuwa maboresho, basi hoja ya ukaguzi haitabaki kuwa kumbukumbu ya tatizo, itakuwa chombo cha kulizuia lisijirudie.

Katika Toleo lijalo, safu hii itachunguza mamlaka na mipaka ya Kamati za Bunge katika kushughulikia hoja za ukaguzi, hususan namna ya kutofautisha kati ya suala la uwajibikaji wa kibunge na suala linalohitaji hatua za kiutawala, kinidhamu au jinai.

# Maswali ya Wabunge: Sauti ya Wananchi Bungeni

**Na**. Athuman Hussein, *ndc*

a.brambati@bunge.go.tz

*"Ishara ya Akili iliyokomaa ni uwezo wa kulichunguza wazo bila kulikubali mara moja"* – Aristoto.

Makala hii ni mwendelezo wa toleo lililopita ambalo lilifafanua dhana, historia, msingi wa kikatiba na kikanuni wa Maswali ya Wabunge, pamoja na nafasi yake katika kuimarisha uwajibikaji na demokrasia. Toleo hili linaendelea kujibu swali: Kwa nini Maswali ya Wabunge yanapewa umuhimu katika shughuli za Bunge?

Mjadala huu unaanzia kwenye kauli: "Kilicho ndani ya kinu, hakitoki bila kutwangwa." Lengo ni kuonesha namna swali linavyoweza kutoka mtaani, kubeba sauti ya mwananchi, kufika Bungeni na hatimaye kuibua majibu, hatua na uwajibikaji wa Serikali.

Mwananchi anapokosa maji haanzi kwa kuandika swali la kibunge. Anaanza kwa kuuliza: Kwa nini maji hayapatikani? Serikali imefanya nini? Tatizo hili litaisha lini? Maswali hayo yanapofikishwa kwa Mwakilishi wa Wananchi, kilio cha mtu mmoja kinaweza kubadilika kuwa swali la umma ndani ya Bunge. Mifano ya Bungeni inaonesha namna mabadiliko hayo yanavyotokea.

Mfano wa kwanza ni Swali Na. 15 lililoulizwa na Mheshimiwa Dkt. Christina Christopher Mnzava, Mbunge wa Viti Maalum, tarehe 1 Novemba 2022. Aliuliza: "Je, nini chanzo cha vifo kwa akina mama wanaojifungua kwa njia ya upasuaji siku chache baada ya upasuaji?" Baada ya kupata jibu, aliuliza maswali mawili ya nyongeza kuhusu upatikanaji wa watumishi wa kutoa dawa za nusu kaputi na kama Wizara ilikuwa imefanya utafiti kubaini dawa zinazosababisha akina mama kupoteza maisha.

Kwa kuwa hakuridhika na jibu la swali la pili la nyongeza, Mheshimiwa Mnzava alisimama kwa mujibu wa Kanuni ya 53(1) ya Kanuni za Bunge, akiomba Mwongozo wa Spika. Tarehe 2 Novemba 2022, Spika alielekeza swali hilo lijibiwe kikamilifu litakapopangwa wakati mwingine. Mfano huu unaonesha kuwa Serikali ina wajibu wa kutoa majibu kamili kwa maswali yanayoulizwa Bungeni, lakini pia unaonesha nguvu ya swali la nyongeza.

Mbunge anapaswa kusikiliza jibu, kubaini pengo na kujenga swali linalolenga kuziba pengo hilo. Hapo ndipo swali linapoanza kubadilika kutoka ombi la taarifa kuwa chombo cha kufuatilia hatua.

Mfano mwingine ni swali la Mheshimiwa Shally Josepha Raymond kuhusu mawasiliano katika Kata ya Uru Kusini. Tarehe 7 Februari 2025 aliuliza: "Je, ni lini sasa tutawekewa mnara katika Kata hiyo ili tuache kukaa kwenye miti kupiga simu?" Swali hili halitosheki na kutambua tatizo; linataka Serikali ieleze hatua itakayochukuliwa na muda wa utekelezaji. Hivyo, nguvu ya swali la aina hii ni kulifanya jambo liwe na hatua inayoweza kufuatiliwa hata baada ya shughuli za Bunge kuahirishwa.

Mheshimiwa Deodatus P. Mwanyika, Mbunge wa Njombe Mjini, naye aliuliza swali la aina hii tarehe 27 Aprili 2026 alipouliza: "Ni lini Serikali itajenga substation kubwa ya Umeme Njombe?" alianza kwa kuunganisha mahitaji ya miundombinu hiyo na maendeleo ya uwekezaji katika eneo hilo kisha akauliza moja kwa moja.

Katika suala la ujenzi wa barabara ya Njombe – Honi - Lusitu, alionesha kuwa barabara hiyo ilikuwa tayari imefanyiwa upembuzi yakinifu na usanifu wa kina, kisha akauliza: "Ni lini sasa Serikali itakamilisha ujenzi wa barabara hii…?" kwa swali hili Mheshimiwa Mwanyika hakulalamikia tu hali ya Barabara bali alionesha kwamba jambo hilo ni sehemu ya ahadi ya Ilani ya Uchaguzi ya Chama Tawala.

Nguvu ya swali hili iko katika neno "itakamilisha", kwa sababu linailazimisha Serikali kueleza hatua ya mwisho na muda wa utekelezaji. Hivyo, swali linaipa Serikali jambo la kufanya na Bunge jambo la kufuatilia.

Swali la Mbunge linaweza pia kuwa chombo cha kubeba sauti halisi ya wananchi. Mwananchi anaweza kukosa nafasi ya kueleza changamoto yake mbele ya Serikali, lakini Mbunge anapoinuka na kuizungumza kwa niaba yake, tatizo binafsi hubadilika kuwa hoja ya umma. Hapo ndipo swali la Mbunge linapopata sura ya uwakilishi wa kweli: si sauti ya Mbunge pekee, bali sauti ya wale waliompa dhamana ya kuzungumza kwa niaba yao.

Mfano mzuri ni swali la Mheshimiwa Faraji Buriani Nandala, Mbunge wa Ndanda, tarehe 13 Aprili 2026 kuhusu fidia kwa wananchi waliopisha njia ya kusafirisha umeme mkubwa kutoka Masasi hadi Mahumbika. Serikali ilikuwa imetenga takriban shilingi bilioni 5.1 kwa ajili ya fidia ya wananchi 1,730.

Badala ya kutosheka na taarifa hiyo, Mheshimiwa Nandala aliuliza: "Ni lini hasa watawalipa hawa wananchi wakati tuko kwenye process za kupitisha bajeti mpya?" Aliendelea kuuliza: "Waendelee kuyaandaa kwa ajili ya kilimo au wasiandae? Na iwapo kuchelewa kwa fidia kutawazuia kutumia ardhi yao, itamgharimu nani kwa kuchelewa huko?"

Hapa ndipo uwakilishi wa kweli unapodhihirika. Kwa mwananchi anayesubiri fidia, suala si tu kama fedha zimetengwa, bali ataweza lini kutumia ardhi yake, kupanga shughuli zake na kuendelea na maisha pasipo kusubiri bila mwisho. Mbunge anapouliza kwa namna hiyo, anampeleka mwananchi Bungeni kupitia swali lake.

Mfano mwingine ni swali la Mheshimiwa Bonnah L. Kamoli, aliyekuwa Mbunge wa Segerea, tarehe 29 Aprili 2025 kuhusu wananchi waliokuwa wakisubiri fidia. Serikali ilikuwa imewalipa wananchi 226 kati ya 1,800. Badala ya kuuliza kwa mtazamo wa takwimu pekee, aliuliza: "Je, Serikali ina mpango gani kuwamalizia hawa wengine, maana wapo kwenye hali mbaya na kuna mvua kubwa zinazonyesha?" Swali hili linaifanya takwimu ionekane kama maisha ya watu halisi mbele ya Bunge.

Lakini swali la Mbunge linaweza kwenda hatua



**nyingine zaidi na kuwa swali linalotafuta uwajibikaji.** Swali la aina hii halitosheki na kujua nini kimetokea au Serikali imefanya nini. Linataka kubaini nani anawajibika, kwa nini wajibu haujatekelezwa na hatua gani zimechukuliwa au zinapaswa kuchukuliwa. Kwa lugha rahisi, linahamisha mtazamo kutoka "Tatizo ni nini?" kwenda "Nani anawajibika kwa tatizo na amewajibishwa kwa namna gani?"

Mfano mzuri ni swali la Mheshimiwa Freeman Mbowe kuhusu utekelezaji wa maazimio ya Bunge. Alianza kwa kuhusisha hoja hiyo na Ibara ya 63(2) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na akataja maazimio mbalimbali, yakiwemo yaliyohusu Operesheni Tokomeza, Escrow na mabilioni ya Uswisi.

Akauliza: "Wewe kama Kiongozi wa Serikali Bungeni, utapenda kusema kwamba Serikali inalidharau Bunge ama Serikali haina majibu ya kutoa?" Swali hili lilihamisha mjadala kutoka kwa nini maazimio hayatekelezwi? kwenda kwenye nani anawajibika kwa utekelezaji wake?

Nguvu ya mfano huu ilionekana pia katika swali la nyongeza. Baada ya Waziri Mkuu kutoa ahadi ya kufuatilia suala hilo, Mheshimiwa Mbowe hakuridhika na kauli ya jumla ya "tutafuatilia", bali aliomba Serikali ipitie Hansard na kumbukumbu za maazimio yaliyopita na ilete Bungeni taarifa ya hali ya utekelezaji. Hapo swali linakuwa chombo cha kufuatilia utekelez

Kuna pia maswali yanayotafuta kioo cha utendaji. Haya hayaishii kutaka kujua kama kazi inafanyika, bali yanataka kujua kiwango, ufanisi na kipimo kinachotumika kutathmini utendaji. Mfano ni swali la Mheshimiwa Naghenjwa Livingstone Kaboyoka, aliyekuwa Mbunge wa Same Mashariki, tarehe 7 Novemba 2018: "Je, Serikali inatumia kigezo gani kutathmini utendaji kazi wa waajiriwa hao kupima ufanisi wao?" Swali hili halilengi kujua tu kama watumishi wapo au wanatekeleza majukumu yao, bali linataka kujua kigezo cha kupima ufanisi wao.

Mfano mwingine ni swali la Mheshimiwa Japhet Ngailonga Hasunga, Mbunge wa Vwawa, kuhusu mfumo wa wazi wa upimaji na ujazaji wa Mkataba wa Utendaji Kazi (OPRAS). Aliuliza: "Je, ni kwa kiasi gani mfumo huu umetekelezwa nchini?" na "Ni lini mfumo wa kupima taasisi (Institutional Performance) utaanzishwa na kuanza kutangazwa hadharani?"

Vilevile, tarehe 4 Septemba 2023, Mheshimiwa Ng'wasi Damas Kamani aliuliza kuhusu ubora wa programu mbalimbali zinazotolewa kwa vijana na matokeo yake. Mifano hii inaonesha swali linalotafuta kipimo cha utendaji, si taarifa tu.

Kwa ujumla, mifano hii inaonesha kwamba Maswali ya Wabunge yanaweza kuhitaji hatua za Serikali, kubeba sauti halisi ya wananchi, kutafuta uwajibikaji au kutaka kioo cha utendaji. Kwa hiyo, swali la Mbunge lisichukuliwe kuwa kauli inayoishia kutafuta jibu. Kwa undani wake, ni zana ya kibunge ya kubeba hoja kutoka kwa wananchi na kuifikisha mbele ya mamlaka yenye dhamana ya utendaji.

Hivyo, ubora wa swali la Mbunge haupaswi kupimwa kwa urefu au uzuri wa maneno, bali kwa uwezo wake wa kuibua ukweli, kubeba sauti ya wananchi, kuleta kipimo cha utendaji na kusogeza uwajibikaji mbele ya Bunge. Hapa ndipo tunapotofautisha kuuliza swali na kujenga swali. Mbunge mwenye umahiri hasimami tu kwenye swali aliloingia nalo Bungeni; anasikiliza jibu, analichanganua na kuamua swali gani linalofuata, ni pengo gani linapaswa kufunguliwa na ni hatua gani inayopaswa kufuatiliwa.

Kwa kuhitimisha, Maswali ya Wabunge ni miongoni mwa njia za kibunge za kufuatilia utekelezaji wa shughuli za umma. Thamani ya swali haiishii kwenye jibu linalotolewa na Waziri. Jibu ni mwanzo wa hatua za kibunge katika kutekeleza madaraka ya Bunge kwa mujibu wa Ibara ya 63(2) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Kwa hiyo, kuuliza Bungeni si kutafuta jibu tu; ni kubeba sauti ya wananchi, kutafuta hatua na kudai uwajibikaji. Kama alivyosema mwanafalsafa na mwanasaikolojia wa Kimarekani, John Dewey: "Tatizo (swali) lililoundwa vizuri ni nusu ya ufumbuzi uliopatikana." **UKWELI UKIZAMA, HAUZAMI MILELE.**





Jarida la Bunge | Toleo la Kumi na Tatu Septemba 2026

# Muswada Kwenye Kamati: Safari ya Kujenga Sheria Bora

**Na.** Athuman Hussein, *ndc*

brambati@bunge.go.tz

*"Mti hauangushwi kwa pigo moja."*

Kama inavyotukumbusha methali hii, jambo lenye uzito halikamiliki kwa hatua moja. Vivyo hivyo, sheria bora haijengwi katika uamuzi wa Bunge wa mwisho pekee, hujengwa hatua kwa hatua kupitia uchambuzi, ukusanyaji wa ushahidi, mashauriano na marekebisho.

Hatua hizo ndizo zinazosababisha Muswada unapofika kwenye Kamati, uchukue maana mpya. Yaani kutoka kuwa pendekezo la sheria kwenda kuwa pendekezo linalopimwa, linalohojiwa na linaloboreshwa kabla ya Bunge kufanya uamuzi.

Hivyo, Muswada kwenye Kamati ni hatua katika mchakato wa kutunga sheria na vilevile ni fursa ya kuupima kwa kina na kujenga ubora wa sheria inayopendekezwa. Katika hatua hii, Muswada huwekwa chini ya uchunguzi wa kina ili kubaini kama dhamira iliyokusudiwa inaweza kutafsiriwa katika masharti ya kisheria yaliyo wazi, yanayotekelezeka na yanayokidhi maslahi ya umma.

Kwenye Kamati kila Ibara hupewa nafasi ya kiudadisi: kwa nini inapendekeza ilivyoandikwa, tatizo gani linakusudiwa kutatuliwa na madhara gani yanaweza kujitokeza baada ya kuwa sheria. Kwa maana hiyo, hatua ya Muswada kwenye Kamati si mwisho wa safari yake, bali ni sehemu ambayo pendekezo la kisera huanza kupimwa dhidi ya uhalisia wa sheria na utekelezaji wake.

Ndiyo maana Kamati haipaswi kutazamwa kama kituo cha kupitishia Muswada kabla ya mjadala wa Bunge. Ni mahali ambapo Muswada unaweza kuchambuliwa kwa jicho la kisheria, kisera, kiuchumi, kijamii na kiutendaji.

Kwenye Kamati, kila kifungu kinachopendekezwa huingizwa kwenye udadisi. Maswali hayo ni kama vile: kwa nini imependekezwa kwa namna hiyo? Tatizo gani inakusudiwa kutatua? na Madhara gani yanaweza kujitokeza baada ya kuwa sheria?

Hapo maswali ambayo huenda hayakuonekana wakati wa uandishi wake wa awali huibuka: Je, kifungu kina maana moja au kinaweza kutafsiriwa kwa namna tofauti? Je, mamlaka yanayotolewa yana mipaka inayotosha? Je, wajibu unaowekwa unaweza kutekelezwa? Je, kuna mwingiliano na sheria nyingine? Na je, suluhisho lililopendekezwa ndilo linalofaa zaidi?

Maswali haya hayalengi kuzuia Muswada kusonga mbele. Yanalenga kuupa nafasi ya kukomaa kabla ya kuwa sheria. Uchambuzi wa Kamati hulifanya Bunge lisitazame tu kile kinachosomeka kwenye Muswada, bali pia kile ambacho Muswada unaweza kusababisha baada ya kuwa sheria.

Katika mchakato huu, Kamati haipati mtazamo mmoja. Wadau wanaweza kuleta uzoefu wa utekelezaji ambao hauonekani katika maandishi ya Muswada, wataalamu hubainisha athari za kiufundi au kisheria na taasisi zinazohusika na utekelezaji hueleza changamoto zinazoweza kujitokeza.

Katika Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ushirikishaji wa wadau umewekewa msingi wa kikanuni. Kanuni ya 139 (9) na 100 (2) za Kanuni za Kudumu za Bunge za mwaka 2025 zinazoweka sharti kwa Kamati kuwaalika wadau.

Waalikwa ni pamoja na wananchi wa kawaida na makundi yenye maslahi katika Muswada, wanaweza kuonesha namna masharti yake yanavyoweza kugusa maisha yao. Kila sauti, inapopimwa kwa umakini, inaweza kuongeza maana na manufaa katika sheria inayopendekezwa.

Serikali nayo huingia katika mchakato huu ikiwa na wajibu wa kueleza na kutetea mantiki ya mapendekezo yake. Kamati inaweza kuuliza kwa nini kifungu kinachopendekezwa kinahitajika, kwa nini mamlaka fulani yanapendekezwa, namna utekelezaji utakavyofanyika na athari zinazotarajiwa. Majadiliano kati ya Kamati na Serikali ni sehemu ya kuhakikisha kwamba dhamira ya kisera inapata tafsiri bora ya kisheria.

Hapo ndipo uchambuzi unapokutana na uamuzi na ushirikishaji wa wadau unapokutana na uwajibikaji. Kamati inaweza kubaini kwamba kifungu kinachopendekezwa kinahitaji kufafanuliwa, kingine kurekebishwa, kingine kuongezwa au pendekezo fulani kuangaliwa upya. Kwa mujibu wa Kanuni ya 100(3) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Kamati inaweza kumshauri Waziri au Mbunge anayehusika kufanya marekebisho katika Muswada.

Katika hatua hiyo Muswada unatoka katika kusomwa na kuelekezwa katika ujenzi wa sheria bora. Marekebisho si kubadilisha maneno kwa ajili ya kuonekana yamebadilishwa, ni kuhakikisha kwamba kile kilichokusudiwa na Muswada kinaweza kufikiwa kwa lugha ya sheria iliyo wazi, yenye uwiano na inayoweza kutekelezwa.

Kwa mantiki hiyo, Muswada unapofika kwenye Kamati, haujaingia kwenye chumba cha kusubiri, bali umeingia kwenye "karakana ya uchambuzi na uboreshaji". Hapa ndipo dhana ya Kamati za Bunge kuwa karakana ya Bunge inapodhihirika katika mchakato wa utungaji wa sheria.

Kimsingi, katika hatua ya Muswada kwenye Kamati, maandishi yanapimwa dhidi ya uhalisia, dhamira dhidi ya utekelezaji na pendekezo la kisheria dhidi ya maslahi ya umma. Shughuli ya Kamati si ya kubadilisha maneno tu bali kuhakikisha kwamba kabla Muswada haujawa sheria, umepewa nafasi ya kutazamwa kutoka pande mbalimbali, kudadisiwa kwa maswali magumu, kupokea maoni tofauti kuhusu muswada na kuboreshwa kwake pale ambapo uchambuzi unaonesha umuhimu wa kufanya hivyo.

Hata hivyo, uchambuzi huo hauanzi na kifungu kimoja kimoja. Kwanza, safari ya Muswada inaanza kwa kuuelewa Muswada wenyewe: kwa nini sheria hii inapendekezwa, tatizo gani inalenga kulitatua na kwa nini njia ya kisheria imeonekana kuwa suluhisho linalofaa. Sheria nzuri haipaswi kuishia kwenye kujibu swali "inasema nini?", inapaswa pia kujibu "kwa nini inasema hivyo?" na "itatumika vipi?"

Baada ya kuelewa dhamira na tatizo linalolengwa, vifungu vinavyopendekezwa huanza kuonekana kwa sura nyingine. Neno moja linaweza kuongeza au kupunguza mamlaka, sentensi moja inaweza kuanzisha wajibu mpya na masharti mawili yanaweza kuonekana kuwa yanakaribiana lakini yakawa na athari tofauti katika utekelezaji. Ndiyo maana uchambuzi wa Kamati hauishii katika kusoma Muswada, unatafuta pia maana, madhara, uhusiano wa masharti yake na mfumo mzima wa sheria.

Katika hatua hii, utaalamu hukutana na wajibu wa kibunge. Wataalamu wa sheria huangalia uhalali, uwazi na ulinganifu wa masharti, wataalamu wa sekta huangalia uhalisia wa utekelezaji, huku watafiti wakileta ushahidi na taarifa muhimu. Kazi ya Kamati ni kuunganisha maarifa hayo na kujenga taswira pana ya sheria inayopendekezwa, kabla ya kufikia uamuzi.

Lakini taswira hiyo haiwezi kukamilika kwa kuitazama sheria kutoka ndani ya Bunge pekee. Ushirikishwaji wa wadau huleta sauti ya uhalisia, changamoto za utekelezaji, gharama ambazo huenda hazikuonekana awali na namna masharti ya Muswada yanavyoweza kuathiri taasisi, shughuli au maisha ya wananchi. Kwa hiyo, kusikiliza wadau si kuongeza tu maoni katika mchakato, bali ni kupanua uelewa wa Kamati kabla ya kufanya uamuzi.

Baada ya maoni na ushahidi huo kupatikana, ndipo kazi ya uchambuzi inapochukua nafasi yake. Kamati haiishii kuyahifadhi kama kumbukumbu, huyaweka kwenye mizani, hutafuta majibu na kuyapima dhidi ya madhumuni ya Muswada, Katiba, sheria nyingine na maslahi mapana ya umma.

Katika hatua hii, uchambuzi huingia zaidi katika masuala ya sera na utekelezaji. Kamati huuliza maswali yanayosaidia kupima uhalisia wa pendekezo: Kwa nini kifungu kinahitajika? Tatizo gani kinakusudia kulitatua? Nani atawajibika kukitekeleza? Gharama zake ni zipi? Na kama hakitatekelezwa kama ilivyokusudiwa, ni changamoto gani zinaweza kujitokeza? Maswali haya si ishara ya upinzani kwa Muswada; ni sehemu ya kuupima kabla haujapewa nguvu ya sheria. Serikali huleta dhamira ya sera, Kamati huleta uchambuzi na maswali.

Kadiri uchambuzi unavyokamilika, hoja, maoni, majibu na mapendekezo huunganishwa ili kuonesha picha ya Muswada baada ya kupitia mchakato wa Kamati. Hapa kazi ya Kamati huingia katika hatua ya majumuisho na kuandaa msimamo unaoweza kuwasilishwa kwa Bunge.

Lakini swali muhimu linabaki: Je, Muswada uliotoka kwenye Kamati ni bora kuliko ule ulioingia? Jibu lake halipaswi kutafutwa katika idadi ya marekebisho pekee. Ubora unaweza kuonekana katika kifungu cha Sheria inayopendekezwa ambacho kimeachwa kama kilivyo kwa sababu uchambuzi umethibitisha uimara wake, katika pendekezo lililokataliwa kwa sababu halikukidhi maslahi ya umma au katika jambo lililofafanuliwa na kuondoa utata unaoweza kujitokeza baadaye.

Hii ndiyo maana uchambuzi wa Kamati haupaswi kupimwa kwa kuuliza tu, "Ni vifungu vingapi vimebadilishwa?" Swali muhimu zaidi ni: "Ni kwa kiwango gani Muswada umeeleweka, umehojiwa na kupimwa kabla ya kupelekwa kwenye uamuzi wa Bunge?" Wakati mwingine thamani kubwa ya uchambuzi haipo katika kile kilichobadilishwa, bali katika uhakika kwamba kile kilichoachwa kimepita kwenye mtihani wa hoja na ushahidi.

Katika hatua hii, kazi ya Sekretarieti nayo huwa muhimu. Hoja za vikao, nyaraka zilizowasilishwa na maelekezo ya Kamati huunganishwa katika kumbukumbu na maandalizi ya Taarifa ya Kamati. Taarifa si simulizi ya kile kilichotokea tu, ni daraja linalobeba matokeo ya uchambuzi kutoka kwenye Kamati kwenda kwenye mjadala wa Bunge.

Taarifa inapokamilika, huwa kama ramani ya safari iliyopita. Inaonesha maeneo yaliyochunguzwa, hoja zilizoibuliwa, majibu yaliyotolewa na mapendekezo ya Kamati. Kwa Wabunge ambao hawakushiriki katika vikao vya Kamati, huwapa fursa ya kuona kazi iliyofanyika kabla ya mjadala wa Bunge. Hata hivyo, Taarifa ya Kamati si mwisho wa mamlaka ya Bunge wala mapendekezo yake si mbadala wa uamuzi wa Bunge. Kamati huchambua kwa kina; Bunge huamua kwa mamlaka yake.

Kwa hiyo, safari ya Muswada kwenye Kamati si safari inayopimwa kwa umbali ulioupita, bali kwa "ubora wa uchambuzi ulioupitia. Kila hatua inaongeza nafasi ya kuuboresha kabla haujafika kwenye uamuzi wa mwisho. Thamani ya kazi ya Kamati haionekani tu katika kile kilichobadilishwa ndani ya Muswada, bali pia katika kile ambacho uchambuzi umeweza kukihakikisha, kukifafanua au hata kukizuia kabla hakijawa sehemu ya sheria.

Kwa mtazamo huo, ushawishi wa Bunge katika kutunga sheria hauishii kwenye kura ya mwisho ya kupitisha au kukataa Muswada. Kama wanavyoeleza Meg Russell na Daniel Gover, "ushawishi wa Bunge hutokea katika mchakato mzima wa sera." Ushawishi huo hujengwa pia katika uchambuzi, maswali, ushahidi, ushirikishwaji na marekebisho yanayoweza kuufanya Muswada uwe bora zaidi.

Kwa hiyo, ubora wa sheria haupimwi kwa uzuri wa maneno yake pekee, bali kwa ubora wa mchakato uliosaidia kuyafikisha maneno hayo katika mfumo wa sheria. Kazi ya Kamati, ingawa mara nyingi hufanyika mbali na macho ya umma, ni sehemu muhimu ya mchakato wa utungaji wa sheria Bungeni. Kwenye Kamati ni mahali ambapo Muswada hupewa nafasi ya kueleweka, kuhojiwa, kupimwa na kuboreshwa kabla ya kuwa sheria.

Ndiyo maana imesemwa, "mti hauangushwi kwa pigo moja" vivyo hivyo, sheria bora hujengwa hatua kwa hatua. Katika hatua hizo, Kamati ni sehemu ambayo Muswada hupewa nafasi ya kukomaa kabla ya Bunge kufanya uamuzi.



# MATUKIO KATIKA PICHA UTHIBITISHO WA MAKAMU WA RAIS BUNGENI




















PARLIAMENT OF TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA

**Jarida hili limeandaliwa na: Ofisi ya Bunge,** 10 Barabara ya Morogoro S.L.P. 941, 40490 Tambukareli, Dodoma.
**Nukushi:** +255 26234218 **Simu**: +255 26 232276-5 **Barua Pepe:** cna@bunge.go.tz

bunge.tanzania Bunge la Tanzania bunge_tz Bunge TV www.parliament.go.tz